

MTINDO KATIKA DIWANI YA MFUKO
MTUPU NA HADITHI NYINGINE

NA
RUTH MUENI KATUTU

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

NOVEMBA 2013

UNGAMO

Tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu chochote.

Katutu Ruth Mueni
(**Mtahiniwa**)

Tarehe: _____

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wateuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Dkt. Amiri Swaleh
(**Msimamizi**)

Tarehe: _____

Dkt. Nyachae Michira
(**Msimamizi**)

Tarehe: _____

TABARUKU

Natabaruku na wazazi wangu, kasisi John Katutu Mutevu na Dorcas Kamende kwa kunilea na kunitia shime ya elimu kila uchao.

SHUKRANI

“Niite, nami nitakujibu na kukuambia mambo makubwa yaliyofichika ambayo hujapata kuyajua.” Wa kuenziwa mwanzo ni Mungu kwa kunipa uhai, nguvu, afya na ujuzi wa kuikamilisha stahiki shahada hii ya uzamili.

Kukamilika kwa tasnifu hii kumefikia kikomo kwa msaada na ushirikiano wa watu kadhaa wa kadhaa. Kwanza natoa shukrani za dhati kwa wahadhiri na wasimamizi wangu, Dkt. Amiri Swaleh na Dkt. Nyachae Michira kwa kuniongoza, kunishauri na kunitia shime wakati nilipokuwa ninashughulikia kazi hii. Mungu awamiminie ujuzi zaidi.

Mbali na hawa, nilinufaika pakubwa kutokana na misaada ya wahadhiri wa idara ya Isimu, hususan kitengo cha Kiswahili walionielekeza na kunidira. Hawa ni Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Evans Mbuthia na Bw.B. Mungania na wataalamu wote katika Idara ya Kiswahili. Mlinifundisha kwa umahiri wa kuigwa na nikafaidika pakubwa. Mungu awabariki sana.

Katika safari hii ya kusaka kubobea katika Kiswahili, kuna wahadhiri wawili wa mwanya ambao walinitia shime na kunipa ushauri ulionifaa sana. Hawa ni Dkt. Hezron Mogambi na Prof. Kineene wa Mutiso. Mungu awajazie baraka zake.

Sitasita kuwashukuru wanafunzi wenzangu kwa mshikamano na upendo tuliobuni tangu mwanzo. Tulijengana na kusaidiana kwa hali na mali huku tukimuenzi Mola kwa yote. Mungu awatizimie ndoto zenu na muendeleo na moyo huo huo wa ujasiri na ukakamavu popote mtakapoenda. Hawa ni Ndumbu Justus, Moraa Lydiah, Chacha Wilson, Muniu George, Perlice

Njeri, Grace Kanyua, Ronoh Jepngetich, Ogutu George, Muriithi Joshua, Nyandago Onyonka, Merolyne Achieng, Keter Peter, Owallah Kennedy, Florence Vutagwa, Lily Chebet, Rose Shikeyi, Paul Motuka, Suakei Ann, Makange Ledemi na Angeline Mainga. Siwezi kuwasahau Mary Nguti na Juliet Okeyo ambao walikuwa nguzo thabiti kwangu katika hali zote. Mungu awafungulie milango yake ya neema.

Shukrani za pekee ni kwa mume wangu Sammy Nzioka kwa upendo na uvumilivu alionitunukia wakati huu. Wengine ni watoto wangu Eric, Mike na Josiah kwa usaidizi na kunielewa wakati nilipoadimika nyumbani. Mwisho ni shukrani za mwanya kwa Jayne Wasike kwa kujitolea kuchapisha kazi nadhifu.

Tasnifu hii imekamilika kwa msaada na ushirikiano na waja wengi ambao siwezi kuwataja wote. Mungu anawajua, awabariki nyote.

ORODHA YA VIFUPISHO

Bi.: Bibi

Bw.: Bwana

Dkt.: Daktari

n.k.: Na kadhalika

Prof.: Profesa

TUKI: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Uk.: Ukurasa

MUHTASARI

Tasnifu hii imeshughulikia mtindo katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Katika sura ya kwanza, mambo muhimu yanayojadiliwa ni; Utangulizi, Tatizo la Utafiti, Madhumuni ya Utafiti, Nadharia Tete, Sababu za Kuchagua Mada, Upeo na Mipaka ya tasnifu, Msingi wa Nadharia ya Utafiti, Yaliyoandikwa kuhusu mada hii na mwisho ni njia tulizotumia kukamilisha utafiti huu.

Katika sura ya pili, utafiti wetu umejikita katika kuchunguza matumizi ya msamiati katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumeshughulikia jinsi mwandishi ameteua msamiati wake ili kuwasilisha ujumbe anaodhamiria kufikisha kwa hadhira yake.

Sura ya tatu inahusu uchanganuzi wa mtindo kwa misingi ya kisintaksia katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumechunguza ukiushi katika baadhi ya kategoria za maneno. Pia tumejadili ukiushi katika sentensi ndefu, fupi na nafasi ya uakifishaji katika sintaksia ya diwani yenyewe. Tumemalizia sura hii kwa kujadili ukiushi unaoibuka kwa kutozingatia muundo wa kiima kiarifa.

Katika sura ya nne, tumechanganua ukiushi wa kisemantiki katika diwani ya kazi hii ya Said Mohamed . Tumechunguza tamathali za usemi kama tashbihi, sitiari, kinaya, tashhisi, tanakuzi, majazi, tasifida, maswali ya balagha na chuku. Pia tumechunguza mbinu nyingine za lugha kama takriri, usambamba wa visawe, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi, jazanda, methali, barua na nyimbo.

Sura ya tano tumehitimisha kwa kurejelea yale tuliyojadili katika sura za awali hasa kwa kuangaza madhumuni, nadharia tete na nadharia tuliyotumiwa kuhakiki kazi hii. Kadhalika

tumeonyesha mchango wetu kutokana na yale ambayo tumeshugulikia katika utafiti huu.
Hatimaye, tumetoa mapendekezo yetu kwa wapenzi wa lugha ya Kiswahili.

YALIYOMO

	Ukurasa
Ungamo	(ii)
Tabaruku	(iii)
Shukrani	(iv)
Orodha ya Vifupisho	(v)
Muhtasari	(vii)
Yaliyomo	(viii)
SURA YA KWANZA	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la Utafiti	3
1.2 Madhumuni ya Utafiti	3
1.3 Nadharia Tete	3
1.4 Sababu za Kuchagua Mada	4
1.5 Upeo na Mipaka	5
1.6 Msingi wa Nadharia	5
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	8
1.8 Njia za Utafiti	10
SURA YA PILI	12
UKIUSHI WA KIMSAMIATI KATIKA <i>MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE</i>	
2.0 Utangulizi	12
2.1 Matumizi ya Maneno ya Lugha Nyingine	12
2.2 Msamiati wa Lahaja ya Kipemba	15
2.3 Uteuzi wa Msamiati wa anwani za hadithi	16
2.4 Ukiushi katika Maumbo ya Maneno	19
2.5 Msamiati wa Sajili	19
2.6 Msamiati Mpya	22
2.7 Hitimisho	24

SURA YA TATU	25
UKIUSHI WA KISINTAKSIA KATIKA MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE	
3.0 Utangulizi	25
3.1 Ukiushi katika mpangilio wa kategoria za maneno katika sentensi	26
3.1.1 Ukiushi wa Nomino	26
3.1.2 Ukiushi wa Vielezi	30
3.1.3 Ukiushi wa Viunganishi	32
3.1.4 Ukiushi wa Vihusishi	36
3.1.5 Ukiushi wa Vivumishi	38
3.2 Sentensi katika <i>Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine</i>	39
3.2.1 Sentensi Ndefu	39
3.2.2 Sentensi Fupi	43
3.2.3 Nafasi ya Uakifishi katika Sintaksia	45
3.2.4 Usambamba wa Kisintaksia	54
3.3 Ukiushi katika Muundo wa sentensi wa Kiima Kiarifu	58
3.4. Hitimisho	63
SURA YA NNE	65
UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE	
4.0 Utangulizi	65
4.1 Tamathali za Usemi	65
4.1.1 Tashbihi	66
4.1.2 Sitiari	71
4.1.3 Kinaya	76
4.1.4 Tashhisi	81
4.1.5 Tanakuzi	85
4.1.6 Majazi	88
4.1.7 Tasifida	91
4.1.8 Maswali ya Balagha	94
4.1.9 Chuku	96

4.2 Mbinu Nyingine za lugha	98
4.2.1 Takriri	98
4.2.2 Usambamba wa Visawe	100
4.2.3 Tanakali za Sauti	102
4.2.4 Kuchanganya Ndimi	103
4.2.5 Jazanda	104
4.2.6 Methali	108
4.2.7 Barua	110
4.2.8 Nyimbo	112
4.3 Hitimisho	113
SURA YA TANO	114
HITIMISHO	
5.0 Utangulizi	114
5.1 Muhtasari wa Utafiti	114
5.2 Mapendekezo ya Utafiti zaidi	116
Marejeleo	117

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Mtindo ni sifa bainifu za kazi fulani hasa kwa kurejelea lugha iliyoandikwa. Fasihi hutumia malighafi ya lugha kufanikisha majukumu yake. Mwandishi husuka lugha kwa namna apendayo ili kupitisha ujumbe wake. Dhana ya mtindo ina fafanuzi kadhaa kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Kuna wale wanaochukulia kuwa mtindo ni mtu. Msokile (1993) akimnukuu Senkoro (1987) anasema kwamba mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kuipa hata kama jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lilelile moja. Mwandishi hutumia tajriba yake ya elimu, uzoefu na hata makaazi kuyasuka maudhui yake kwa njia ya upekee ili kuzuka na uyeye katika kazi fulani.

Mohamed (1995:44) anauchukulia mtindo kama jumla ya tabia za lugha za kikundi au wakati fulani. Kuna uwezekano wa kikundi fulani katika kipindi fulani kifupi au kirefu kuwa na mtindo fulani wa uandishi. Kwa mfano, tunaweza kuzungumzia ushairi wa Kiswahili wa karne ya 18 au 19 au mtindo wa ushairi wa kisasa. Mwandishi haandiki Kiswahili cha insha ya darasani, lakini Kiswahili kama anavyokisikia yeye kikizungumzwa sehemu alizozioea yeye. Ingawa kuna upekee wa uandishi, kipindi fulani cha wakati huelekea kuathiri waandishi wa kipindi hicho hicho na hivyo kuandika kazi ya kimtindo inayofanana.

Mtindo pia huchunguzwa kama uteuzi. Mwandishi huteua msamiati wake maalum kimaksudi au pasina maksudi. Huweza kuchagua neno moja na kuacha kisawe chake ili

liafiki muktadha anaozungumzia. Topan(1971:22) anasema kwamba, uandishi ni jambo la uchaguzi kwa vile mwandishi huchagua kuandika neno hili na kuacha neno lile. Kwa vile uchaguzi huu hufanywa kwa sababu maalum, basi kile kinachoandikwa nacho huwa na sababu maalum. Lugha moja inayobeba takriban ujumbe unaofanana lakini yenye maumbo tofauti ya maneno huweza kuwasilishwa kwa mitindo tofauti kutegemea uteuzi wa maneno ya mwandishi.

Mtindo pia unaangaliwa kama ukiushi wa kaida. Kila lugha ina miundo yake inayokubaliwa na kuitawala katika rejesta mbalimbali. Kinachoangaliwa ni jinsi msamiati au maneno yanavyotumika. Mohamed (1995) anasema mtindo huu hutoa thamani kwa miundo inayojitokeza kwa ugeni na upya. Wamitila (2008: 354) anakubaliana na haya kwa kusema kinachochunguzwa ni uteuzi wa msamiati mpya na uliopo, miundo na mipangilio ya sentensi, neno au sauti, uteuzi na matumizi ya tamathali za usemi na jazanda na hata sifa za uakifishi zinazoelekea kukiuka njia za kawaida za kuakifisha.

Dhana hizi zote zinaingiliana pakubwa kwani mwandishi wa kazi fulani ya fasihi huteua maneno yake na kuyaeleza kwa namna anayotaka. Katika kujieleza, aghalabu huchota maudhui yake kutoka kwa jamii anamoishi. Msamiati wake unapobainika kuwa una ugeni na upya, husemekana ni ukiushi wa kawaida. Mkabala wetu ni kwa mtindo ni ukiushi wa matumizi ya lugha.

Kwa misingi hiyo, maoni yetu ni kwamba Said A. Mohamed ametumia mtindo unaobainika wazi katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Ametumia ufundi wake wa maneno ili kusuka na kuwasilisha maudhui yake kwa njia mwafaka na mpya.

1.1 Tatizo la Utafiti

Vipengele mbalimbali vya kimtindo vimetumiwa kuendeleza maudhui katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Said A. Mohamed ametumia mtindo kwa upekee fulani kutokana na jinsi alivyoiteua na kutumia lugha. Hiki kimekuwa kichocheo kikubwa kwetu kuchunguza upekee huu katika kazi hii.

Diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* ilichapishwa mnamo mwaka wa 2005. Uchunguzi wetu umebainisha kuwa diwani hii haijahakikiwa na mtaalamu yeyote kuonyesha jinsi mbinu za kimtindo zimefaulisha maudhui yake. Hivyo basi, kwa kuchagua kuchanganua mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*, tumeliziba pengo hilo na kutoa mchango wetu wa kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili.

1.2 Madhumuni ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

- (i) Kuhakiki vipengele muhimu vya kimtindo katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.
- (ii) Kubainisha jinsi ukiushi wa vipengele vya kimtindo unaendeleza maudhui katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.
- (iii) Kubainisha athari za muumano wa mtindo na maudhui katika uelewekaji ujumbe katika diwani *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

1.3 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- (i) Mwandishi amefaulu kutumia vipengele vya mtindo kwa upekee katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.
- (ii) Mwandishi amefaulu kutumia vipengele vya kipekee vya kimtindo katika kuendeleza maudhui katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

(iii) Diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* imebainisha uelewekaji wa athari za muumano wa mtindo na maudhui unavyofaulisha ujumbe.

1.4 Sababu Za Kuchagua Mada Hii

Suala la mtindo limehakikiwa sana katika tanzu za fasihi kama tamthilia, riwaya na ushairi. Wahakiki wachache ndio wameshughulikia mtindo katika hadithi fupi. Wamitila (2004) anakiri kuwa si vitabu vingi vya hadithi fupi vilivyochapishwa kufikia sasa nchini Kenya. Hili limetupa msukumo wa kuhakiki diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Katika uchunguzi wetu, hatujapata ushahidi wowote kuthibitisha kuwa kuna uhakiki wowote wa kina uliokwisha kufanyiwa diwani hii kwa upande wa jinsi mtindo unavyoendeleza maudhui. Utafiti wetu umeliziba pengo hili.

Tumeshughulikia diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* kwa sababu ni kazi ya mwandishi mmoja, Said A. Mohamed. Kazi hii imetupa mwongozo wa mtindo katika kuchunguza baadhi ya hadithi zilizomo. Hii ni tofauti na diwani za hadithi fupi ambazo huwa na hadithi za waandishi tofauti tofauti. Diwani hizi ni pamoja na *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine* (2000), *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004,) miongoni mwa diwani nyingine. Waandishi wa hadithi zilizomo wametoka katika maeneo mbalimbali na wanaiakisi mitizamo anuwai ya maisha na jinsi ya kuuwasilisha uhalisia. Mitazamo na mitindo hii tofauti itakuwa changamoto kubwa katika kuzihakiki kitaalamu.

Mwandishi huteua lugha yake kwa uangalifu ili iwe yenye mvuto na mnato kwa wasikilizaji au wasomaji wake ili washawishike na ujumbe anaotaka kupitisha. Mwandishi hutumia mtindo kama gari tegemewa la kuwasiliana na wasomaji wake. Mintarafu ya uzito wa

wajibu wake, tumehakiki mtindo katika diwani hii ili kuonyesha ufaafu wake katika kuwasilisha maudhui.

1.5 Upeo na Mipaka

Said. A. Mohamed ameandika diwani tatu za hadithi fupi. Diwani hizi ni *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine* (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005) na *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005). Tumechunguza jinsi mtindo unaendeleza maudhui katika diwani.

Kwa kuchagua diwani moja ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*, tumeweza kuhakiki kwa kina mtindo wa hadithi zilizomo. Tumechanganua matumizi ya lugha katika kiwango cha sintaksia, semantiki na msamiati na kuweka wazi mtindo wa baadhi ya hadithi zilizomo.

Tumechanganua matini yetu katika viwango vitatu ambavyo ni ukiushi wa kimsamiati, ukiushi wa kisintaksia na ukiushi wa kisémantiki.

1.6 Msingi wa Nadharia

Uhakiki wetu wa mtindo katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* umeongozwa na nadharia ya Elimumitindo. Kwa mujibu wa Wamitila (2008:504), Umitindo kama anavyoita nadharia hii, hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha maarifa ya isimu na huweza kuelezwa kama nadharia ambayo iko katikati ya isimu na fasihi. Kimsingi, nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa matini za kifasihi. Leech na Short (1981:13) wanafasili nadharia ya Elimumitindo kama uchunguzi wa mtindo. Wanafasili Elimumitindo kama jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na mtu fulani na kwa lengo mahususi. Kufafanua zaidi dhana hii, waliegemea mawazo ya Ferdinand de Saussure, mwanaisimu wa Uswisi. Mwanaisimu

Ferdinand alitofautisha mfumo lugha (*yaani langue*) na matumizi lugha (*au parole*). Mfumo lugha ni jumla ya kanuni za lugha ambazo hutumiwa na wazungumzaji wa lugha fulani. Matumizi lugha nayo ni hali halisi ya usemaji kutoka kwa kanuni ambazo wazungumzaji au waandishi hutumia katika mazingira tofauti. Watumizi huchagua maneno fulani na si mengine kama matumizi yao ya kila siku na kufanya mtindo kuelekea kuwa matumizi lugha (*parole*).

Uchanganuzi wa nadharia ya Elimumitindo ulikua mwishoni mwa karne ya ishirini. Wawakilishi wa shule ya Prague wa fasihi ndio walioweka misingi ya Elimumitindo.

Waasisi wa Urasimu ndio waliokuwa wana Elimumitindo wa kwanza. Lakini kazi yao haikueleweka huko magharibi kwa sababu ya athari ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka 1917. Baada ya vita, Roman Jacobson aliondoka Urusi na kuhamia mji wa Prague ambapo alikuwa mwanachama wa 'The Prague Linguistic Circle' ambao walishughulika zaidi na jinsi fasihi iliathiri wasomaji. Yeye na wanaisimu wengine kama I. A. Richards walikataa uhakiki wa fasihi uliojikita zaidi kwa mwandishi. Walichukua mwelekeo uliochunguza jinsi uhakiki wa fasihi ulivyomwathiri msomaji kwa sababu ya maumbo mbalimbali ya kazi fulani. Wanaisimu hawa na wengine wakaibuka na kukuza kile kilichoitwa Nadharia ya Uchimuzi (*foregrounding*). Mtazamo huu ulikariri kuwa sehemu fulani za fasihi andishi zinaathiri wasomaji zaidi ya sehemu nyinginezo. Sababu ni kuwa sehemu hizi huwa na ukiushi fulani usiozowewa ambao huzifanya zijiitokeze zaidi kwa wasomaji.

Jacobson akahamia Marekani kutoka Prague na kuendeleza msimamo huu wake wa Elimumitindo na ukastawi nchini Uingereza na Marekani.

Nadharia hii inashughulika na wepesi au uchangamano katika sanaa ya usemaji au matini za kifasihi kwa kuangalia maneno, virai na ruwaza za sentensi na ufaafu wake katika matumizi yake. Unadhamiria kuzichanganua matini za kifasihi kwa kuuchunguza mtindo kwa njia ya “kisayansi”.

Mbatiah (2001:11-12) anasema kuwa uhakiki wa kimtindo hujaribu kubainisha sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi ya kifasihi, maandishi ya msanii au kipindi mahsusi. Sifa hizo zinaweza kuwa za kifonolojia (kiwango cha isimu kinachoshughulikia ishara na sauti za lugha Fulani), kisintaksia (dhana ya Isimu inayochunguza miundo ya sentensi na mpangilio wa vipashio katika sentensi), kimsamiati (maneno dhahania na maneno thabiti, kuwepo na idadi fulani ya nomino, vielezi, vivumishi n.k.) au kitamathali (sifa ya kibalagha ya tamathali za usemi, urudiaji, jazanda n.k.).

Wamitila (2008:512) anachangia sifa hizi kwa kuziita viwango. Anaongeza kusema kuwa kuna kiwango cha kimaandishi au grafolojia (suala la uakifishaji, mpangilio wa aya (au ukosefu wake) n.k., kiwango cha kifonetiki (kiwango cha lugha kinachoshughulikia ishara-sauti zinazopatikana katika lugha), kiwango cha kimofolojia (tawi la isimu linalochunguza viungo vya maneno na kuonyesha jinsi viungo hivyo vinavyoambatana kuunda maneno mapya) na kiwango cha kisemantiki (kuhusu maana ya maneno na sentensi, aghalabu kuna aina mbili, maana dhahania na maana husishi).

Wafula na Njogu (2007:101) wanasema kuwa baadhi ya sifa na viwango vya lugha ya kiisimu humsaidia mhakiki kuichambua kazi ya fasihi. Kwa mfano, moja kati ya sifa bia za lugha ni utata. Lugha inaweza kueleza jambo moja kwa njia nyingi kwani ina uwezo wa

kuvuka vizingiti vingi kimaana. Mhakiki ana jukumu la kubainisha na kuchanganua utata kama kipengele kinachomwezesha mwanasanaa kutumia maneno machache kuwasilisha dhana pana au kutumia maneno mengi kuwasilisha maana ndogo.

Nadharia ya Elimumitindo wakati mwingine hukanganya kwa kuitwa Elimumitindo ya kifasihi au Elimumitindo ya kiisimu. Inaitwa Elimumitindo ya kifasihi kwa sababu inaelekea kuangazia matini za kifasihi. Kwa upande wa pili, inaitwa Elimumitindo ya kiisimu kwa sababu zana zake muhimu huchotwa kutoka kwa isimu. Elimumitindo inaweza kutumika kama dhana ya kijumla inayohusu uchanganuzi wa lugha nyingi za kifasihi au sajili; upeo huu mpana wa Elimumitindo unakaribiana na kazi zinazofanywa katika Isimu jamii. Maarifa yanayotokana na isimu hutumiwa ili kubainisha sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi.

Katika utafiti wetu, hatujashughulikia vipengele hivi vyote; haiwezekani kuvichunguza vyote kwa undani. Tumechunguza ukiushi wa kimsamiati, kisintaksia na kisemantiki katika mpangilio wa vipashio katika sentensi.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kitsao (1975) amehakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili katika tasnifu yake ya ‘A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts’. Amefafanua mtindo kwa kuchunguza namna mbalimbali za kueleza mtindo. Kwa mfano, mtindo kama upekee wa mtu, mtindo kama matumizi ya lugha, mtindo kama namna ya kujieleza, mtindo kama uteuzi wa maneno na mtindo kama ukiushi wa kaida. Baada ya kufanya hivyo, amechunguza namna mtindo unavyodhihirika katika kazi mbalimbali za kifasihi

anazozitafitia. Kazi hizi ni sehemu chache za tafsiri ya Julisi Kaizari, hadithi fupi za Kiimbila J. K. katika *Visa Vya Ulimwengu* na *Simu ya Kifo* na *Wasifu wa Siti bin Saad* ya Shaaban Robert. Mhakiki huyu amechunguza mtindo katika kazi nyingi, sisi tumehakiki katika kazi moja. Yeye amelinganisha riwaya mbili, sisi hatujalinganisha. Uhakiki huu umetufaa kwa kutupa mwangaza katika kushughulikia suala la mtindo katika tasnifu yetu.

Ndung'u (1996), katika tasnifu yake 'Uhakiki na fani katika riwaya za Katama Mkangi', amechunguza vipengele vya mtindo na kutathmini kufaa kwa matumizi yake. Pia amechunguza maudhui katika; *Ukiwa* (1975), *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu ametafitia vipengele vya kimuundo, ploti na wahusika ambavyo sisi hatujatafitia. Mhakiki huyu amechunguza fani katika utanzu wa riwaya, sisi tumechunguza utanzu wa hadithi fupi. Kwa upande mwingine, mwelekeo wake umetufaa katika kuhakiki katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Otieno (2005) amehakiki kipengele cha mtindo katika tasnifu yake "Muumano wa Leksika katika matini: *Babu Alipofufuka*. Amesema kwamba, baada ya msanii kutambua maudhui ya kazi yake, huchunguza lugha ya matini ili kufafanua uteuzi wa tamathali za usemi akichanganua upekee wowote ule wa mtindo wa msanii. Amesema kuwa msanii huwa huru kukiuka kaida za ruwaza ya lugha ili kuchangia uwiano unaonata.

Tasnifu hii imeshughulikia uchunguzi wa kiufafanuzi wa muumano wa leksika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* kwa kutumia nadharia ya usasa na usasaleo, umuundo na nadharia isimu-mtindo. Sisi tumechunguza suala la mtindo katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* na wala si riwaya. Tasnifu yetu imejikita katika nadharia ya Elimumitindo.

Mchango wake katika kufafanua mtindo umetufaa katika kuchunguza jinsi mtindo wa *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* umeendeleza maudhui yake.

Ongarora, (2007) ameshughulikia mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Ameangalia mtindo kama matumizi ya lugha. Amehakiki ukiushi katika mpangilio wa nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihusishi katika sentensi. Tena ameangazia baadhi ya ukiushi wa kisemantiki na mbinu nyingine za lugha katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Diwani hii haijahusisha jinsi mtindo unavyoathiri maudhui kama vile tumefanya katika kazi yetu. Hata hivyo, uchanganuzi wake ni muhimu kwa kuwa umetupatia mwanga wa kuhakiki mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Kitali (2011) ameangalia fani katika tamthilia mbili, *Pango na Mama Ee*. Amechunguza jinsi wahusika wanawake wanavyotumia lugha. Katika kipengele cha mtindo, ameangalia mbinu za lugha zilizoteuliwa na mwandishi kama zimemkuza ama kumdunisha mwanamke. Yeye amejikita katika fani za matumizi ya lugha, wahusika, mtindo, mandhari usimulizi na sauti inayosimulia kazi hii. Sisi tumejikita katika vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo ni vya kisintaksia, kisemantiki na kimsamiati. Kitali ametafitia tamthilia, utafiti wetu umetalii utanzu wa hadithi fupi. Hata hivyo, utafiti wake umetufaa kwani tumetumia baadhi ya vipengele vya mtindo alivyotumia yeye ili kuonyesha jinsi vimeendeleza maudhui katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

1.8 Njia za Utafiti

Utafiti wetu ni wa maktabani. Tumedurusu tasnifu tofautitofauti, vitabu na makala mbalimbali yanayohusiana na mada yetu. Pili tumefanya upekuzi wa kina katika tovuti mbalimbali kwenye mtandao kuhusiana na suala la mtindo. Tumesoma kwa uangalifu

diwani ya *Hadithi Fupi ya Mfuko Mtupu* na *Hadithi Nyingine* maana ndio msingi wetu wa kushughulikia yanayohusiana na somo letu. Nne, tumewashirikisha wahadhiri wetu, wataalamu wa fasihi pamoja na wanafunzi wenzetu katika mijadala kuomba ushauri wao kila ilipohitajika. Data yote imechanguliwa kwa misingi ya nadharia ya Elimumitindo.

Katika sura ya pili, tumeanza uchanganuzi wetu kwa kuchambua ukiushi wa kimsamiati katika kazi hii ya Said A. Mohamed.

SURA YA PILI

UKIUSHI WA KIMSAMIATI KATIKA MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumemulika jinsi mwandishi ametumia msamiati katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Maana ya msamiati sio maneno magumu katika lugha bali ni jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Mwandishi ana uhuru wa kuteua msamiati wake anavyotaka, uhuru wa kuchagua neno moja na kuliacha lingine. Uhuru huu ndio humtambulisha mwandishi na kumtofautisha na mwingine.

Msamiati hufungamana na matukio, masuala na mazingira katika kazi fulani. Mohamed ameeleza maana ya baadhi ya msamiati katika sehemu ya sherehe katika diwani hii. Katika sura hii, tumechunguza matumizi ya maneno ambayo si ya Kiswahili sanifu, msamiati wa lahaja ya Kipemba, anwani za hadithi, ukiushi wa maumbo ya maneno, msamiati wa sajili na msamiati mpya.

2.1 Matumizi ya Maneno ya Lugha Nyingine

Mwandishi ametumia mtindo wa kuyachukua maneno ya Kiingereza kama yalivyo na kuyatumia katika hadithi bila kuyabadilisha. Baadhi ya maneno hata ameyafungia katika alama za mnukuu (‘ ’) na mengine ameyaandika kwa herufi za mlazo. Mtindo huu unaitwa kuchanganya ndimi.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, mwandishi anaonyesha ukengeushi wa Saada kupitia kwa maneno haya:

Usiku huu ulikuwa na mbalamwezi:

Hakuna jingine hapo pao shambani.

Kwa masaa yale aliyofika Bumbwisudi

amechoshwa na kutamani lini kuche aende

mjini. Ziko wapi Bumbwisudi zile pirikapirika

za usiku wa Ulaya? Ziko wapi ‘bars’, ‘night’

clubs? Ziko wapi ‘theatres’ na sinema? Ziko

wapi mandari, parties na 'ma-disco'?

(uk.34)

Neno 'bars' kwa Kiswahili ni baa, mahali pa kuuzia na kunywa pombe, neno 'night clubs' ni vilabu vya usiku, neno 'theatres', ina maana ya majumba au viwanja vya maonyesho (au tamthilia). Maneno 'parties' na 'ma-disco' kwa Kiswahili ni dhima au karamu na disko, mtawalia, katika Kiswahili sanifu. Huu ni mtindo wa mwandishi unaongeza unakshi wa kazi yake na kubainisha maudhui ya kukengeuka kwa Saada zaidi.

Katika hadithi ya 'Njia Fupi', Naima anajikwatua sawasawa kwa rangi ya mdomo, podari, kujirashia mafuta mazuri, kuzikoleza kope wanja na kadhalika. Anajikwatua hivi kabla ya kwenda kwa Mama Kitimbi ambapo anapanga kumnasa mume wake Fumu katika tabia zake za uzinzi. Tunasoma:

Mipango kapanga mwenyewe, hakuna
sababu asiitekeleze mwenyewe
na kuona taathira yake mwenyewe.
Naam, hakujali. Aliazimia kuchukua
'time' yake, huku kunuwia taathira
kuikuza na ikibidi shadda na madda
kwa makusudi ya kumwona simba
anayemtega kaingia mtegoni.
(uk. 131).

Neno 'time' limetumika badala ya neno 'wakati' la Kiswahili sanifu ili kuonyesha jinsi Naima Mambo hakuwa na haraka yoyote katika mpango wake wa kumtega na kumnasa Fumu katika jumba la Mama Kitimbi. Anataka aabike na kuacha tabia yake ya uzinifu.

Katika hadithi ya 'Hukumu', tunasoma:

Kufumba na kufumbua mahabusi
wetu alitekwa kitikiti na kutupwa
nyuma ya gari kubwa la waya
na kufuli ikabanwa. Matwana
akajumuika na mahabusi wenzake
waliokuwa wakienda mahkamani.
Humo walibaki kuchungulia kwenye
matundu ya waya kama wanyama
kwenye 'zoo'.
(uk. 141)

'Zoo' ni neno la Kiingereza lenye maana ya bustani au mahali wafungwapo wanyama wa pori kulingana na *English-Swahili Dictionary* (2006). Mwandishi ametumia neno hili kimaksudi ili kuonyesha dhuluma ya Matwana ya kunyimwa uhuru wake kama wanyama pori wanaofungiwa pamoja. Yeye na wafungwa wengine wanaelekea mahakamani kujibu mashtaka mbalimbali.

Katika hadithi ya 'Pigo Kupokezana', Mtama anajiambia kuwa yaliyompitikia kwa muda wa miaka saba katika ndoa yake ni mengi. Tunasoma:

Na mambo mengine
kinehe! Huwaje yeye
kumpa uzi wa roho
yake mtu mwingine
auchezee?
(uk. 22)

Neno 'kinehe' lina maana ya 'mno' au 'kupita kiasi' kwa lugha ya Kinyamwezi. Ufafanuzi huu ni kwa mujibu wa sherehe ya mwandishi mwenyewe. Mateso ya Mtama kutoka kwa Daudi mumewe yamepita kiasi, anaamua kuyakomesha.

2.2 Msamiati wa Lahaja ya Kipemba

Katika baadhi ya hadithi, mwandishi ametumia baadhi ya maneno ya lahaja hasa Kipemba.

Wandao na wenzake (2007) wanasema kuwa lahaja ni kimojawapo katika ‘vilugha’ mbalimbali vya lugha moja vinavyobainika kijamii au kijiografia na vinavyotofautiana kwa vipengele maalum vya kisauti na kimuundo.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, baada ya Mfuko Mtupu kuangusha gilasi na kuamriwa na mwenye mkahawa aondoke, anakataa. Wateja wanamtambua. Tunasoma:

Mfuko Mtupu, bwana
mmoja aliyekuwa akila
humo mkahawani
aliongeza. Mwendawazimu
‘uyo’, alihitimisha mwenye
mkahawa.
(uk. 4)

Neno ‘uyo’ ni lahaja ya kipemba ambalo lime doneshwa silabi ‘h’ kumrejelea Mfuko Mtupu na vitimbi vyake.

Katika hadithi ‘Mhanga wa Mwanamaua’, maelezo kuhusu Kipelele yanatoa picha halisi ya ng’ombe huyu aliyekuwa tayari kupigana. Tunasoma:

Linafoka. Linatoka kipovu
cha kinywa. Limeinua
masikio. Limesimamisha
mkia. Katoa macho
yanayomwaa. Linaangazia
mara huku mara huku.
(uk. 83)

Neno ‘yanamwaa’ ni neno la lahaja ya Kipemba lililo na maana ‘yanayomng’ara’. Macho ya Kipelele yanang’ara kwa hamu ya kumhujumu mtu. Kumchezea Kipelele ni mchezo hatari unaosababisha kifo cha Dadi. Mwandishi anaupinga.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, Fumu anashuhudia mapodozi ya mkewe kutokea kichwani hadi nyayoni. Fumu analambatia mate anapoangalia ‘macho malegevu kwa usingizi wa mapenzi’ (uk.122) ya mkewe. Tunasoma kuwa:

Mikono mabega na mabilinganyi ya
kwapa na mtutumko wa mwili
umedhihiri, kumfanya Fumu wakati
huu maji aite mma.
(uk. 132)

‘Mma’ ni msamiati wa Kipemba unaorejelea ‘maji’ kama watamkavyo watoto wadogo wanaojifunza lugha yao. Mwandishi anasema kuwa umbo la kuvutia la mkewe lilimsusua Fumu mpaka akaanza kubambanya maneno kama mtoto mdogo. Mwandishi anapinga ulafi wa wanaume wanaoacha wake zao warembo wakifuata makahaba.

2.3 Uteuzi wa Msamiati wa Anwani za Hadithi

Mwandishi Said Ahmed Mohamed ameteua anwani za hadithi zake kwa ufundi mkubwa ili zioane na maudhui ya hadithi zake.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, anwani hii ina maana kuwa mtu anapokupiga, nawe mpige ili muwe sawa. Dawa ya kichapo ni kichapo, anasema. Katika hadithi hii, Mtama anavumilia pigo la mumewe kwa muda mrefu. Anapigwa magumi na mateke na Daudi bila kuteta. Anapoamua kuchukua hatua, anameza dawa za kumfisha uhai kwa muda ili atathmini athari ya ‘kifo’ chake kwa mumewe. Kipigo hicho kinamuathiri Daudi hadi anaomba msamaha kutoka

kwa mkewe na wanaishi kwa mapenzi na amani. Kichwa hiki kinachochea watu wachukue hatua kubambe ili kuzua mabadiliko katika maisha yao.

Anwani ya ‘Tumba Iliyovia’, ni cha sitiari. Mbatiah (2001:75) anasema kuwa sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi ambapo vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile vinahusianishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mojawapo ya maana ya tumba ni ‘ua linalofumba kabla ya kuchanua’; nacho kitenzi ‘via’ kina maana ya kudumaa, kushindwa kufikia kiwango kinachotakiwa katika ukuaji wa kiumbe. ‘Tumba Iliyovia’ ni ua ambalo limeshindwa kuchanua. Tumba ni sitiari ya Saada katika hadithi. Wazazi na wanakijiji wa Bumbwisudi wanakuwa na matarajio ya juu kuhusu msaada ambao Saada angewapa baada ya kwenda Ulaya kusomea uwakili. Wazazi wake wanatarajia kuwa angewajengea jumba la fahari waache kuishi katika kibanda chao cha mgongo, angewanunulia shamba, mifugo na kuimarisha maisha yao ya uzeeni. Kwa Wanabumbwisudi, Saada angekuwa alama ya fahari, wangejivunia wanakijiji jirani, kuwa Saada, aliyebeba ujuzi wa Ulaya ametoka kijiji chao. Saada anaporejea, ndoto hizo zinavia. Saada amebadilika, kimaumbile na kimavazi hadi wazazi wanaona aibu kumtazama. Anakataa kuwasabahi na hata kuwasalimia. Saada anarejea mjini usiku huo huo. Ndoto za wazazi zilizojikita kwake zinadumaa. Wanakijiji pia hawamwonei fahari kwa sababu anawaambia kuwa yeye si waziri ndipo awasaidie kujenga shule. Matumaini yao kwake yamevia. Saada amekataa kuchanua kuwasaidia wanaomtegemea. Anwani ya hadithi ya mwandishi inafiki ujumbe. Matukio ya hadithi hii yanaonyesha asante ya mateke ya Saada kwa wazazi na wanakijiji wa kwao.

Katika hadithi ya ‘Nyumba ya Pazia’, Sheikh Majid anamkosoa Kassim kwa kunywa pombe na kushirikiana na wasichana kimapenzi. Baadaye, Kassim anagundua kuwa Sheikh Majid ni

mnaifiki kwani ni mpenda wasichana huku akijivika joho la ushehe. ‘Nyuma ya Pazia’, ni nyuma ya yale maneno matupu ya kushauri, kumbe nyuma yake Sheikh ni mnaifiki. Anwani hii inakuza maudhui ya unafiki.

Hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, ni kwelikinzani, yaani ukweli wenye ukinzani. Mwendawazimu huwa hana akili timamu. Kichwa cha hadithi hii kinaashiria mwendawazimu mwenye akili timamu, au mwenye ujuzi. Tunasoma, ‘Shati, imechanikachanika, lakini safi kama kioo. Inang’ara hata uliweza kujiona juu yake. Tabia hii ya kujipekua na kuchungua unadhifu wa mwili na nguo zake, Mwenda imemganda tokea ujana wake.’ (uk.111).

Kwa kawaida, mwendawazimu anayezurura mjini huwa mchafu kupindukia. Mwenda ni mwendawazimu mwenye akili maana ni nadhifu. Tena, jina lake lilikuwa Mwenda. Alipofika mjini siku ya kwanza akiwa amevalia mararu, watoto walimrushia mawe na kumwita ‘Mwendawazimu’. Tangu siku hiyo jina likamganda. Akawa anacheka ovyo ili kuficha uchungu uliomkaa moyo wa kupoteza mkewe na mwanawe Siraba. Vicheko vyake pia vinamsaidia kuuthibitishia ulimwengu kuwa alikuwa mwendawazimu, lakini alikuwa mwendawazimu mwenye akili.

Anwani ya ‘Njia Fupi’ inaaifiki tabia ya ulaghai na uasherati wa Fumu ambaye hatimaye anagunduliwa na mkewe. Fumu anamuacha mkewe mrembo Naima na kwenda danguro la Mama Kitimbi kutafuta makahaba. Naima anapogundua siri hii, anajikwatua kweli kweli na kujipeleka huko danguroni kama mmoja wa makahaba. Fumu anapokimbilia huko kutuliza joto lake la mwili, anamkuta huko. Njia ya uwongo wake ikawa fupi, mkewe anamgundua na kumwaibisha. Njia yake ni fupi. Anwani hii inaasa kuwa, uwongo huwa haudumu.

2.4 Ukiushi Katika Maumbo ya Maneno

Umbo ni sura ya jinsi mtu au kitu kilivyokaa au kilivyoumbwa. Sifa moja ya msamiati wa Mohamed ni kwamba, maneno mengi yameandikwa kwa mtindo wa mlazo au italiki. Arege (2007:300) anasema kuwa herufi za mlazo kama anavyoziita hutumiwa kuyabainisha au kuyapambanua maneno yanayohitajika katika kifungu au maelezo. Mohamed anatumia italiki kupambanua mawazo yake katika baadhi ya maneno. Maneno haya yaliyoandikwa kiitaliki yanafafanuliwa katika sherehe. Huu ni mtindo wake wa kukiuka mazoea ya uandishi.

Mbali na kutumia italiki, Mohamed vilevile anakoleza baadhi ya maneno katika baadhi ya hadithi zake. Kwa mfano, katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, neno ‘**nikikunyari**’ (uk.59). Katika barua ya ‘Maryam Abdulla’ kwa Sheikh Majid neno hili limeandikwa kwa herufi kama hii. ‘Nikikunyari’ ina maana ya ‘nikikutazama kwa makini’, ambalo ni la lugha ya mtaani. ‘Maryam’ alilitumia ili kuongeza hamu ya Sheikh kukutana naye ili amwaibishe.

2.5 Msamiati wa Sajili

Wandao na wenzake(2007) wanasema kuwa sajili au rejista ni matumizi ya lugha katika mazingira au miktadha mbalimbali. Lugha hii, hubadilikabadilika kwa mujibu wa mazingira au shughuli ya mahali penyewe. Mwandishi ametumia sajili mbalimbali katika hadithi zake.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ mazingira ni ya mkahawani. Kwa hivyo tunasoma msimulizi akimwambia mhudumu pale, ‘Hebu, mletee mzee huyu pilau sahani moja...’(uk. 6). Yeye alikuwa akila pilau hii. Maneno ya msimulizi yanaonyesha ukarimu wa baadhi ya wanajamii kwa wenzao.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, mwandishi ametumia sajili ya mashambani kuelezea usuli wa Saada. Tunasoma:

Kwa muda wote huo, walimeza
mrututu huku wakiota ndoto
ya kuvunja kile kibanda chao
cha mgongo; wakanunua shamba
lao ambalo dakika hiyo lilikuwa
kikataa tu. Wakainunua mifugo
na kuimarisha maisha yao ya
uzeeni.
(uk. 30)

Haya ni matumaini ya wazazi wa Saada wakiota jinsi Saada angewafaa atakaporudi kutoka Ulaya. Angewanunulia shamba na ng’ombe. Hii ni sajili ya mashambani.

Kwingineko katika hadithi hii, Miraji anamwambia Saada:

Saada, umekuwa ng’ombe asi
aliekata kamba na kumwagaa
ovyo katika mbuga za kutisha
usiku na mchana? Ulikuwa
waridi lisilo miba.
(uk.35)

Miraji anatumia sajili ya shambani kuonyesha utundu wa Saada, anatumia ng’ombe asi na waridi lisilo miiba. Sajili hii inabainisha peupe malezi na utoto wa Saada kabla ya kwenda Ulaya. Sajili ili imetumiwa ili kuonyesha kiasi kikubwa cha mabadiliko ya Saada ya kupapia tabia za ugenini huku akiacha ya kwao.

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’, kuna sajili ya mapenzi katika mazungumzo baina ya Mwanamaua na Dadi. Tunaelezwa kuwa Mwanamaua ana mambo mawili yanayomsumbua. Tunaelezwa kuwa Dadi aligonjea kwa hamu atwikwe mzigo wowote bila kujali uzito wake, madhali mtwikaji ni Mwanamaua. Tunasoma maneno ya Mwanamaua:

Unajua kwamba mimi ninakupenda
na nimekubali kuolewa na wewe
miongoni mwa vijana wote wa kijiji
hiki. Na wewe unatambua kwamba
niliwakataa na kuwaepuka wote.
(uk. 80).

Mwanamaua anamfahamisha Dadi kuwa alivutiwa na huruma, ucheshi, ukakamavu na uhodari wake wa kazi. Maneno haya ya mapenzi ndiyo yanamwaminisha Dadi kuwa angeweza kumchezea Kipelele na kushinda ingawa hakuwa amewahi kucheza tena. Sajili hii inaonyesha nguvu za ushawishi wa mwanamke unaoweza kumtia mwanamme pabaya.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, kuna sajili ya mahakamani. Tunasoma:

Mshitakiwa Matwana Kusi,
tarehe 28/3/82, mnamo saa
9 za alfajiri, iligundulikana
maiti ya Uledi wa Haji
katika konde yako. Kesi
ilifika mahkamani na wewe
kushukiwa kuwa ndiye
uliyemhujumu Uledi kwa
visu mpaka akafa. Kesi
ilisikilizwa kwa muda wa

mwezi mzima na
kuthibitika kwamba wewe
ndiye mwuuaji wake.
Mahkama ilikupa fursa
ujitete kama haki
inavyoamuru.
(uk. 141-142)

Maneno yaliyopigiwa mstari ni ya sajili ya mahakamani na yanaoana na hadithi ya Matwana anayeshitakiwa kwa makosa ya kumuua Uledi.

2.6 Msamiati Mpya

Msanii ana uhuru wa kubuni msamiati mpya usiokuwepo katika lugha ili kuonyesha ubunifu wake na pia kutosheleza mahitaji yake ya kuendeleza maudhui.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, Mtama anaishi kwa masimango na kisirani cha kila siku kutoka kwa mumewe. ‘Mtama aliugopa usiku kama mduma!’(uk.24). ‘Duma’ ni aina ya chui wa kiafrika anayefanana na chui, ni kiumbe kinachokimbia kwa kasi na kinachotisha. Daudi analinganishwa na mnyama huyu kwa sababu ya vitendo vyake katili. Mwandishi ameongezea silabi ‘m’ mwanzoni mwa neno duma na kuzua ‘mduma’. Kawaida neno hilo huwa halina kiambishi hiki. Huu ni ubunifu wa msamiati mpya wa mwandishi Mohamed.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda alizurura mjini akishuhudia vituko vya dunia. Wakati mmoja mvulana mmoja anayefuatana na msichana anapomhadharisha asisogee alipokuwa Mwenda kwa sababu ni mwendawazimu, Mwenda anasita na kuwaangalia. Tunasoma, ‘Mwenda alitupa maklobu yake ya macho kwenye miguu ya huyo mwanamke’(uk.107). Mwandishi ametumia neno ‘maklobu’ kwa maana ya ‘macho makubwa’

katika muktadha huu. Huu ni msamiati mpya wa macho kutoka kwa huyu msanii mwenye ubunifu mkuu.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, mwandishi anaelezea kwa kina mapambazuko ya alfajiri ya siku ya Matwana kufikishwa mahakamani. Kwa Matwana ni asubuhi ngumu akiwana na nafsi yake iwapo angesema ukweli wa muuaji wa Uledi au la. Mtafaruku wa fikira zake unatiliwa nguvu na milio ya huzuni ya wanyama asubuhi hii. Tunasoma:

Baadaye komba alililia kwa
mlio wa huzuni kabisa. Mara
panya walibumburisha kama
vile wakiwania kitu kwa
kinyang’anyiro. Mara nyingine
paka walifukuzana katika
hamkani zao za uchuro,
wakamnyaua na kupapurana.
(uk. 138)

‘Wakamyaua’ ni kitenzi ambacho mwandishi ameunda kutokana na mlio wa paka wa miyau yao. Paka hulia ‘nyau’, ‘nyau’. Huu ni msamiati unaombainisha mwandishi kati ya wengine. Unasaidia uelewekaji wa mtafaruko wa ukinzani katika nafsi ya Matwana. Milio hii ya wanyama ni taashira ya mtafaruku wa hisia za Matwana unaoelekeza kubashiri hatima ya kesi yake. Alihukumiwa kifo.

2.7 Hitimisho

Katika sehemu hii tumeangazia msamiati wa Mohamed katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumeona jinsi mwandishi alivyotumia msamiati kwa upekee fulani. Tumechunguza

matumizi ya maneno ya lugha nyingine, msamiati wa lahaja ya kipemba, uteuzi wa anwani za hadithi, ukiushi wa maumbo, msamiati wa sajili na msamiati mpya.

Msanii Mohamed ametumia msamiati kwa ufundi mkuu ili kupitisha maudhui yake. Ufundi wake unakiuka misingi na sheria za lugha tambuliwa za jambo. Linakuza uelewekaji wa kazi yake kwa kiwango kikubwa. Katika sura ya tatu inayofuata, tumechanganua matini kwa kuangalia ukiushi wa kisintaksia.

SURA YA TATU

UKIUSHI WA KISINTAKSIA KATIKA *MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE*

3.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia sintaksia katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Obuchi na Mukhwana (2010:136) wanafasili sintaksia kama kitengo cha kimuundo ambacho hushughulikia sentensi katika lugha. Sintaksia, kama utanzu wa isimu, hushughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazounda sentensi kama vile kategoria za maneno, virai na vishazi. Sintaksia hushughulikia muundo wa sentensi kwa kuchunguza viambajengo vyake pamoja na kanuni na sheria zinazofuatwa katika uundaji wa sentensi na viambajengo vyake mbalimbali.

Madhumuni yetu ni kuchunguza jinsi mwandishi amekiuka matumizi ya kawaida ya mpangilio wa maneno ili kuupitisha ujumbe wake. Ili kufanikisha hili, tumetoa mifano ainati ya ukiushi, athari za ukiushi na jinsi umechangia kuyajenga maudhui kwa uwazi zaidi. Tena tumeonyesha namna sentensi zingeandikwa katika hali yake ya kawaida. Uchunguzi wetu umefanikishwa kwa kutalii kategoria mbalimbali za maneno kulingana na utendakazi wake katika sentensi au mahala pa kila neno katika tungo. Kategoria hizi ni pamoja na nomino, vielezi, viunganishi, vihusishi, viwakilishi, vitenzi, vivumishi na vihisishi.

Mbali na kutalii kategoria za maneno, tumejadili urefu na ufupi wa sentensi za mwandishi. Tumetoa mifano kadhaa inayoonesha usanii wa mwandishi katika kukuza maudhui yake.

Fauka ya hayo, tumeangazia nafasi ya uakifishi wa mwandishi katika diwani yake. Tumbainisha ni alama gani za uakifishi alizotumia zaidi, kwa nini na namna zinavyoathiri sintaksia katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Jambo lingine ambalo tumechunguza ni jinsi mwandishi alivyogawa sentensi zake kulingana na uamilifu wa kishemu hicho. Kimapokeo, sentensi hugawika kwenye kiima na kiarifu kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana(2010:179). Kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hueleza yule anayetenda au anayehusika na kitendo fulani. Sentensi yoyote haikamiliki pasina kiima (nomino au kiwakilishi chake). Kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo hutoa taarifa kuhusu kiima, hutaja jambo linalofanywa na kiima au linalofanyiwa kiima. Tumechunguza ukiushi wa kiima kiarifu katika sentensi alizounda mwandishi katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

3.1 Ukiushi Katika Mpangilio wa Kategoria za Maneno Katika Sentensi

Massamba (2004) anasema kuwa sarufi miundo ni taaluma ya isimu ambayo hujishughulisha na uchunguzi na uchanganuzi wa mahusiano yaliyopo kati ya maneno katika tungo. Lugha ya binadamu hufuata utaratibu ambao unaongozwa na sheria maalum za kiisimu ili kuunda sentensi au tungo zenye maana. Hatujachunguza kategoria zote kama zilivyotajwa hapo juu bali tumeangazia vipashio vya; nomino, vielezi,viunganishi, vihusishi na vivumishi.

Tumeangalia jinsi mwandishi amekiuka sheria za uundaji katika kuteua sentensi zake na jinsi utokawaida huu unaathiri sintaksia katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

3.1.1. Ukiushi wa Nomino

Nomino ni maneno yanayotaja vitu, viumbe, hali, mahali, vyeo na matendo. Kihore na wenzake (2000:86) wanafafanua zaidi kwa kusema kuwa katika uamilifu, nomino hufanya kazi ya kukipambanua au kukibainisha kitajwa kwa muungano wa madhumuni ya kukitofautisha na vitajwa vingine. Katika lugha ya Kiswahili, sentensi kamili huundwa kwa muungano wa kiima na kiarifu. Kiima ni sehemu ya sentensi inayokaliwa na nomino au kikundi nomino. Kiarifa hutoa taarifa kuhusu kiima hicho. Kwa kawaida, kiarifu huja baada ya kiima. Kiarifu hubeba

viambajengo mbalimbali kama shamirisho na chagizo. Shamirisho husimamia nomino au kikundi cha nomino ambacho hujaza nafasi ya mtendwa au mtenda katika sentensi. Obuchi na Mukhwana (2010: 171) wanasema kuwa shamirisho hutokea baada ya kitenzi. Chagizo husimamia neno au kikundi cha maneno kinachojaza nafasi ya kielezi au vielezi katika tungo na sentensi. Baadhi ya sentensi katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* zimetumia shamirisho mahali ambapo si pake na huu unakuwa ni ukiushi.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunasoma:

“Mimi nahitajia kulipwa”, alisema huku
kaviringa ngumi na kuuma meno, “Mimi
itanilipa nini jamii hii? Enh, itanilipa nini?”
(uk.4)

Kwa kawaida, sentensi hii ingekuwa:

Jamii hii itanilipa nini mimi?

Mwandishi ameiandika ilivyo ili kusisitiza kuwa mwalimu Mfuko Mtupu anailaumu jamii kwa shida zake zote kama za kuishiwa na pesa, mke kumtoroka na kutojua mtoto wake alikokuwa.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, tunasoma:

Yeye Mtama alitaka iwe huzuni
ya moja kwa moja atakapoipata Daudi.
(uk. 25).

Nomino ‘Daudi’ imewekwa mahali si pake. Huu ni ukiushi. Mwandishi ameiweka hapo ili tuelewe kuwa Mtama, mkewe Daudi, amechoshwa na magumi na mateke ya mumewe. Anataka

atende jambo kama kujiua ili Daudi ahuzunike. Vitendo vyake vya kulipiza kisasi vingeelekezwa kwa Daudi. Katika usemi wa kawaida tungetarajia sentensi hii iandikwe hivi:

Yeye Mtama alitaka iwe huzuni
ya moja kwa moja Daudi atakapoipata.

Katika hadithi ya ‘Kicheko Cha Mwendawazimu-Akili’, tunasoma:

Alisimanga kimoyomoyo Mwenda.
(uk.107).

Nomino ‘Mwenda’ inawekwa mwisho katika sentensi badala mwanzo kama ilivyo kawaida ya kikundi nomino. Kuiweka pale ni kuongeza ujumi wa lugha na kuonyesha lawama alizonazo Mwenda kwa msichana na mvulana wanaompita na kumwita mwendawazimu. Kawaida, sentensi hii ingekuwa:

Mwenda alisimanga kimoyomoyo.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, tunasoma:

Uchu Fumu ulikuwa umemshika
(Uk. 133)

Fumu anashuhudia mkewe Naima akijirembesha chumbani mwao. Naima alikuwa ametimua shore kichwani, amepaka uso wake podari, macho ameyaimarisha kwa wanja mweusi na midomo yake imerembwa kwa rangi ya waridi. Mapambo haya yanamwacha Fumu hai akimlambatia mate mkewe.

Ndiposa neno ‘uchu’ linaanzia sentensi ili kusesitiza hamu ya Fumu. Huu ni ukiushi kwa sababu nomino hizi mbili hazifai kufuatana. Sentensi hii ingeliandikwa:

Uchu ulikuwa umemshika Fumu.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, tunasoma:

Na jambo hili Matwana aliamini.
(uk.137).

Kwa kawaida sentensi hii huandikwa:

Matwana aliamini jambo hili.

Ukiushi huu una athari ya kumulika zaidi mawazo ya Matwana kuhusu unyanyasaji wa wanyonge unaotekelezwa na walio na nguvu. Matwana anaamini kuwa sheria inawapendelea wenye mali huku ikiwatenga wasio navyo na kuwasingizia uhalifu. Sentensi ya mwandishi inazua uzito unaotarajiwa.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, kuna mfano mwingine wa ukiushi wa nomino. Mwandishi anasema:

Mambo haya yanakwenda kwa
siku nyingi mpaka mwenyewe
Uledi habari akazipata.
(uk.144).

Badala ya kuandika nomino ‘Uledi’ mwishoni wa sentensi, mwandishi anaiandika kabla ya kitenzi ‘akazipata’. Mwandishi anataka kusesitiza kuwa Uledi hatimaye alipata kujua kuwa Bwana Hakimumu anayetaka kumfunga kwa kifo cha Uledi, ndiye hasa muuaji. Anataka kusesitiza kuwa Uledi ndiye alikosewa. Katika hali ya kawaida sentensi hiyo ingekuwa:

Mambo haya yalikuwenda
kwa siku nyingi mpaka
Uledi mwenyewe akazipata
habari.

3.1.2 Ukiushi wa Vielezi

Kulingana na Massamba (2004: 31), kielezi ni neno au tungo yoyote itumikayo kutoa maelezo zaidi juu ya kitenzi, kivumishi au hata kielezi kingine. Kwa kiasi kikubwa, vielezi hueleza zaidi kuhusu kitenzi; tendo limefanywa kwa jinsi gani, kwa masharti gani, wapi, kwa chombo gani na katika mazingira yapi. Kuna mifano kadhaa ya ukiushi katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ kuna mawazo ya msimulizi kuhusu mhusika Mfuko Mtupu. Msimulizi anataka kumnunulia sahani ya pilau baada ya kumkagua na kuiona hali yake. Kabla hajafanya hivyo, Mfuko Mtupu anamuuliza anataka kufanya nini, uso wake ukiwa umejaa kiburi cha kusema yeye hakuwa mwombaji. Msimulizi katika fikra zake akasema, hisia za uso huweza kudanganya. Tunaelezwa:

Huyu hapa mtu mwenye uwezo wa
kumfadhili binadamu mwenzake.
(uk.2-3).

‘Hapa’ ni kielezi cha mahali. Kinasisitiza uwepo wa msimulizi kuwa eneo moja na Mfuko Mtupu. Kielezi hiki kinaelezea zaidi kuhusu kivumishi ‘huyu’ kuonyesha haja ya msimulizi ya kumsaidia kwani alikuwa karibu naye. Sentensi hii ingekuwa:

Mtu huyu hapa mwenye uwezo
wa kumfadhili binadamu mwenzake.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’ tunaelezwa jinsi Mtama hakuweza kukata pingu za utumwa wa ndoa yake. Anajisabilia mwili na roho kupigwa na kutusiwa na mumewe Daudi kwa ajili ya

watoto wao wawili, Zamda na Riziki. Kila siku akawa anajiambia atajikomboa. Tunaelezwa kuwa:

Akabaki anajisabilia katika nguvu
zilezile anazotaka kuziepuka lakini
anazozifia roho. Kesho, kesho kutwa,
mtondo na mtondogoo.
(uk, 23).

‘Kesho, kesho kutwa, mtondo na mtondogoo’ ni vielezi vya wakati.

Mwandishi amevifuitanisha vyote ili aonyeshe kuwa kila siku Mtwana anaahirisha ari yake ya kujikomboa. Ukiushi mwingine ni kuwa vielezi hivi havielezi kuhusu vitenzi, vivumishi wala vielezi vingine. Huu ni ukiushi kwa sababu sentensi kamili, ni lazima iwe na kiima na kiarifu; hii haina.

Aidha, katika hadithi hii tunaelezwa kwamba siku hii Mtama ameamka vibaya. Tunasoma:

Leo Mtama lakini aliamka vibaya. (uk.25)

Leo ni kielezi cha wakati kinachofaa kuelezea zaidi kuhusu kielezi ‘vibaya’. Mwandishi amekiweka mwanzo ili kusisitiza kuwa siku hii na si nyingine, Mtama ameamua kuchukua hatua ili akomeshe dhuluma ya mumewe kwake. Pia kuna ukiushi wa kiunganishi lakini. Kikawaida, ‘lakini’ ndilo lingekuwa mwanzo wa sentensi hii. Sentensi ingesomeka:

Lakini, Mtama aliamka vibaya leo.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’ tunasoma:

Usiku ule Matwana hakupata usingizi
(uk.137)

Matwana amekaa jela kwa muda wa mwezi mmoja kwa mashtaka ya kumuua Uledi rafiki yake. Kwa mwezi huo wote, hajitetei ingawa nafasi anapewa. Usiku wa kuamkia kukatwa kwa kesi yake, anaamua kuongea: ndiposa mwandishi anasisitiza hili kwa kutanguliza sentensi kwa kielezi ‘usiku ule’ cha wakati. Kawaida, sentensi ingefaa kuwa:

Matwana hakupata usingizi usiku ule.

Aidha katika hadithi hii tunaelezwa:

Leo hapa lakini mahkama inataka
kutoa hukumu ya kuwa mimi muuaji
bila ya kueleza hata kisa cha mimi
kuua... (uk.143).

Kielezi ‘leo’ ni cha wakati na ‘hapa’ ni cha mahali.

Mwandishi anachimuza maneno haya ili kuisitiza kuwa siku hii, mahakama inataka kumhukumu Matwana bila ushahidi wa kutosha. Haijapata ushahidi wa kutosha kwa mwezi mzima. Kikawaida sentensi hii ingekuwa:

Lakini mahakama inataka leo hapa
kutoa hukumu ya kuwa mimi muuaji
bila ya kueleza hata kisa cha mimi kuua.

3.1.3 Ukiushi wa Viunganishi

Viunganishi ni maneno yenye kuunganisha vipashio mbalimbali katika lugha. Huunganisha maneno, virai, vishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali ya viunganishi. Kuna viunganishi

nyongeza kama vile: na, tena na pia, viunganishi visababishi kama vile: kwa hivyo, kwa kuwa, basi, kwa sababu, kwa maana n.k. Viunganishi vya masharti kama: ikiwa, endapo na kama; viunganishi viteuzi kama vile ama, au, wala na aidha; viunganishi vya wakati kama halafu, kisha na hatimaye viunganishi vya kinyume kama vile lakini, ingawa, ijapokuwa n.k. Mwandishi amekiuka matumizi ya viunganishi katika sentensi. Ametumia sana kiunganishi ‘na’ kama mtindo wake. Sentensi nyingi zinaanza kwa ‘na’ ambao ni ukiushi kwa sababu ‘na’ inastahili kuunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi na sentensi na sentensi.

Katika hadithi hii hii, tunasoma:

Mambo yalifikia mfundani hatimaye. (uk.1)

Haya ni maelezo ya msimulizi anapoeleza hisia alizokuwa nazo siku nyingi kuhusu Mfuko Mtupu. Anahisi zimefika mwisho na kaamua kufanya jambo. Ndiposa kiunganishi hatimaye kinakamilisha sentensi yake. Kwa kawaida, kiunganishi hatimaye kingeanzia sentensi hivi:

Hatimaye mambo yalifika mfundani.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ tunasoma:

Mara alijivuta tena mbele, kwa ghafla vilevile,
akajisogeza kwa kasi na kuilalia meza. Na
mimi nikaemewa, mkono wangu ukiwa
umeng’ang’anaa ndani ya sahani ya pilau
(uk.2)

Msimulizi anataka kumuagizia Mfuko Mtupu sahani ya pilau. Anapoinua mkono ili amwite mhudumu, ghafla Mfuko Mtupu anajisogeza mbele na kuilalalia meza. Msimulizi anatumia kiunganishi na kuanza sentensi kuelezea kwamba vitendo vya Mfuko Mtupu havikutarajiwa.

Aidha, katika hadithi hii anauliza:

Sikudhani kama nilikuwa na haki ya
kutaka kumsaidia. Na ni jambo gani
hasa lililonisukuma?
(uk.2)

Mwandishi anaanza sentensi kwa kiunganishi ‘na’ bila kuonyesha vipashio viwili anavyoiunganisha.

Katika hadithi hii hii ya ‘Pigo Kupokezana’ mwandishi amekiuka mtindo wa mpangilio kubalifu wa maneno kwa kuanza sentensi kwa kiunganishi cha uteuzi ‘wala’. Anasema:

Wasaa ni masafa kama utampa Mtama
afunge virago vyake na kupiga mbio
kokote atakako. Wala si pande la bahari
kama atapiga mbizi na kuibuka ng’ambo
nyingine.
(uk. 22).

Dunia ya Mtama ya mateso katika ndoa haimpi idhini ya kufunga virago na kwenda anakotaka wala si bahari ya kupiga mbizi kwenda ng’ambo ya pili. Kiunganishi ‘wala’ hutumiwa kuonyesha vitenzi viwili ambavyo havikukamilika katika sentensi moja. Mwandishi hapa amekiuka matumizi ya lugha.

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’ tunasoma hivi:

Na iwe vyovyote vile, jina la
Mwanamaua limemsibu!
(uk.76)

Hii ni sentensi ya kwanza ya hadithi hii na mwandishi ameanza kwa kiunganishi ‘na’. Anataka kutilia mkazo ufaafu wa jina la mhusika Mwanamaua kwamba anapendeza. Kivutio kingine ni kuwa hili ni jina la kinga analokabidhiwa msichana anapozaliwa kisiwani Pemba. Mwanamaua amevutia wanaume wengi kwa urembo na tabia yake. Mwandishi anaanza kwa kiunganishi ‘na’ kama mtindo wake.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, tunaelezwa:

Na sasa katatizwa. Nguvu mbili
zilikuwa zikizongana kichwani.
Naima! Kwa Mama kitimbi!
(uk.133)

Naima anamwacha mumewe Fumu chumbani mwao bila kumwambia wazi anakoenda. Fumu anatatizika asijue amfuata mkewe ajue mipango yake au aende kwa Bi. Kitimbi. Mwandishi anaanza sentensi kwa kiunganishi ‘na’ bila kuonyesha sehemu mbili za neno, virai au vishazi vinavyounganishwa. Huu ni ukiushi ili mwandishi achochee Fumu aende kwa Bi. Kitimbi ili uozo wake kumwendea kinyume mkewe ujulikane.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’ tunasoma:

Alitamani awe na wakili, lakini
alijua kwamba maskini kama
yeye asingemlipa wakili katika
nchi hii. Wala mahkama hii haitoi
wakili wa bure kumtetea mtu kama
yeye.
(uk.142).

Kiunganishi ‘wala’ huunganisha vitenzi viwili visivyowezezana kama ilivyoielezwa awali. Msanii anapoanza sentensi kwa ‘wala’ kuonyesha kwamba Matwana hangetetewa na wakili kwa sababu mbili; umaskini wake na mahakama kutotoa wakili wa bure, huu ni ukiushi wa viuganishi.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, tunasoma:

Alijibu Matwana kwa sauti yake,
tanda kabisa, kisha akakipa nafasi
kimya kieneze taathira. Ndipo
tena akaendelea. “Lakini utafanyaje
unyonge unapokuelemea?”
(uk.142)

Matwana alikuwa mahakamani akijitetea kuwa hukumua Uledi, rafiki yake. Mwandishi ameanza sentensi kwa kiunganishi ‘lakini’ kwa sababu anatoa sababu ya kauli aliyotoa awali ya kunyamaza kwake mwezi mzima. Umaskini ulimzuia.

3.1.4 Ukiushi wa Vihusishi

Kihusishi ni neno linaloonyesha uhusiano baina ya neno moja na jingine au maneno au uhusiano kati ya kitu na kitu kingine au kati ya mtu na kitu au hata hali. Maneno yanayotumika kama vihusishi ni kama kati ya, juu ya, mbele ya, kando ya, nyuma ya, upande wa, mkono wa, tena, mpaka, hadi, kwa, kuliko n.k.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunasoma:

Nyuma ya mzee Mfuko Mtupu kwenye
uwazi wa madirisha yaliyozibwa
waya na kuchomea mahindi, nzi
walikuwa wakitapia kuingia.
(uk.5).

‘Nyuma ya’ ni kihusishi ambacho kimetumiwa mwanzoni mwa sentensi. Katika dondoo hili, msanii amekitumia ili kutoa msisitizo wa mahali nzi walipokuwa. Haya yanaonyesha maudhui ya uchafu wa mkahawa huu. Huu ni ukiushi kwa sababu katika kanuni za sarufi ya Kiswahili, kihusishi hakitumiki mwanzoni mwa sentensi. Sentensi ingefaa kuandikwa:

Nzi waliokuwa nyuma ya mzee
Mfuko Mtupu kwenye uwazi
wa madirisha yaliyozibwa waya
wa kuchomea mahindi walitapia
kuingia.

Mfano mwingine unapatikana katika hadithi ya ‘Hukumu’ ambapo tunasoma:

... akasadikisha kwamba mfungwa
mmoja anamwonea mwenzake.
Hata kati ya wafungwa kwa
wafungwa kuna kuoneana...
(uk.139).

Mwandishi ameanza sentensi kwa kihusishi ‘hata’ kuonyesha maudhui ya maonevu hayapatikani katika mahakama tu, pia miongoni mwa wafungwa wenyewe. Sentensi hii ingeandikwa:

Kuna kuoneana hata kati ya wafungwa
na wafungwa.

Hadithi hii pia ina ukiushi mwingine wa kihusishi pale mwandishi anapoandika:

Matwana alingoja. Kwa muda alihisi kimya.
(uk.139).

Ameanza sentensi kwa kihusishi 'kwa'. Matwana anangojea askari waje ndani ya seli ili wampeleke mahakamani kwa hukumu. Alikuwa amesikia hatua za viatu zikikaribia mlango wake. Sentensi ingestahili kuwa:

Alihisi kimya kwa muda.

Kuanza kwa kihusishi 'kwa' kunaongeza taharuki ya usomaji kutaka kujua kilichoendelea mahakamani. Je, Matwana angefungwa?

3.1.5 Ukiushi Katika Matumizi ya Vivumishi

Kulingana na Massamba (2004:39), kivumishi ni neno linalotoa taarifa zaidi juu ya nomino inayohusika. Kuna vivumishi aina mbalimbali kama: vivumishi vya sifa, vya idadi, viulizi, idadi, virejeshi, vimilikishi n.k.

Katika hadithi ya 'Pigo Kupokezana', tunasoma:

Hata hivyo siku zote hizo aliuma meno,
akajiachia achomwe mikuki ndani ya
moyo wake.
(uk.24).

Mtama anamruhusu mumewe ampige kila siku kwa ajili ya watoto wake. Mwandishi anasisitiza utukiaji wa dhuluma kwa kuanza kwa kivumishi kiashiria 'hizo'. Huu ni ukiushi katika mtindo wake. Mwafaka zaidi ingekuwa:

Hata hivyo siku hizo zote
aliuma meno, akajiachia
achomwe mikuki ndani ya
moyo wake.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’ kuna ukiushi huu wa mpangilio wa maneno yanayojumuisha vivumishi. Tunasoma:

Je, akisema ukweli, itanusuru
roho yake hii inayotaka
kudhulumiwa? Afanye nini?
(uk.138)

Matwana ana mvutano wa ndani kwa ndani akijiuliza iwapo ataiambia mahakama ukweli au juo kuhusu kifo cha Uledi au la. Je, ule ukweli ungemzuia kutofungwa? Msanii anakiuka katika mpangilio wa vivumishi viwili anavyotumia mfululizo vikirejelea roho ya Matwana. Kivumishi kiashiria ‘hii’ kingetangulia halafu kifuatwe na cha umiliki ‘yake’. Sentensi ingekuwa:

Je, akisema kweli, itanusuru
roho hii yake inayotaka
kudhulumiwa? Afanye nini?

3.2 Sentensi Katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*

Obuchi na Mukhwana (2010) wakimnukuu Crystal (1991) wanasema kuwa, sentensi ni kipashio cha kujieleza kinachosheheni fikira kamili. Said Ahmed Mohamed amechanganya sentensi fupi na ndefu katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* kama mtindo wake wa kujieleza.

3.2.1 Sentensi Ndefu

Hakuna idadi kamili ya maneno inayotengewa sentensi ndefu. Hata hivyo, unapokumbana na sentensi ambazo zimetumia maneno zaidi ya thelathini, zinanata hisia. Tumezichukulia kama ukiushi wa kimtindo wa msanii. Urefu wa sentensi hizi hufanikishwa kwa matumizi ya

viunganishi kama ‘na’, ‘wala’, ‘lakini’, ‘au’, ‘kama kwamba’, ‘halafu’, na ‘tena’. Virejeshi kama ‘amba’ vimetumiwa pia.

Mohammed (1995: 107) anasema kuwa urefu wa sentensi huzifanya kudorora na kujikokota katika mtitimo au tempo ya utaratibu. Hali hii ya udororaji na uzorotaji wa sentensi inaumana na maana ya huzuni, wasiwasi, msiba, uvivu wa jambo au kulizia ndege mbaya. Pia huweza kutumika katika mbinu ya usimulizi au mahubiri. Mwandishi anapooanisha sentensi ndefu na maana ya maudhui yanayojengwa, usanii wake hujitokeza dhahiri.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunaambiwa:

Lakini nilipokuwa naivuta hii aaaaa,
niligundua mzee ghafla ameshituka,
akarudi nyuma ya kiti na kujiachia
huko huku akizidi kung’arisha
macho yake meupe makubwa
ambayo yalikuwa yamemezwa
kwenye mashimo yake.

(uk.1).

Sentensi hii ndefu imeunganishwa kwa viunganishi ‘na’, ‘lakini’ na ‘huku’ na kirejeshi ‘ambayo’. Sentensi hii inajikokota na kuashiria wasiwasi na huzuni wa Mfuko Mtupu. Alikuwa amefika kwenye mkahawa na kukaa mbele ya msimulizi wa hadithi hii.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’ tunasoma:

Daudi aliona hisia ngeni zikimpanda
ndani ya nafsi yake, hisia alizokuwa
nazo kabla hajamuoa Mtama na
ambazo kwa muda mrefu zilikuwa
ama zimejificha pahala fulani ndani
ya nafsi yake au basi tu zimepotelea
pahali fulani asipopajua.
(uk.27).

Viunganishi ‘na’, ‘ama’, ‘au’ na kirejeshi ‘ambazo’ vimetumiwa ili kuunda sentensi hii ndefu. Sentensi hii inaashiria kudorora kwa mtitimo au tempo ya hadithi baada ya Daudi kugundua kuwa mkewe Mtama alikuwa ‘maiti’. Mtitimo unapunguzwa na huzuni inayomkumba.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’ , tunasoma:

Na ulipokuja wakati wa kukitia shule,
juu ya watu wake kumcheka
kuwa alikuwa mjinga kupoteza mali
yake kwa kumsomesha mwanawe na
kumpa elimu, kitu kisichoonekana wala
kukamatika, yeye alipiga moyo konde,
akasema potelea mbali atamsomesha
Siraba mpaka awe daktari.
(uk.117).

Viunganishi ‘na’ na ‘wala’ vimetumiwa kuunda sentensi hii.

Tempo ya sentensi hii inadorora wakati msimulizi anaregesha hadithi nyuma kueleza sababu na mbinu alizotumia Mwenda kumsomesha mwanawe Siraba.

Aidha, katika hadithi hii tunaambiwa:

‘Mzee Mwenda, huyu ni Siraba mwanao,
amekuja jana jioni kutoka Köln Ujerumani,
na baada ya kufika nyumbani bila ya
shaka amekuta aliyoyakuta na ameyasikia
aliyoyasikia, basi amemlilia Mzee Josef
amlete kwako, naye Mzee Josef kwa kujua
akifika kwangu amefika kwako, ndio
kamleta, na sisi tumekufuata.

(uk.119)

Viunganishi ‘na’ na ‘basi’ vimetumiwa kuunganisha viambajengo mbalimbali vya sentensi hii ndefu. Sentensi hii ndefu inaonyesha kujikokota na kupunguzwa mwendo wa hadithi kwa maana ni muhtasari wa maisha ya Mwenda ya miaka ishirini. Siraba, mwanawe Mzee Mwenda, alienda Köln Ujerumani kusomea udaktari miaka ishirini nyuma ya siku hii. Mwenda, aliuza ng’ombe na shamba ili apate karo. Siraba hakurudi wala kuwaandikia barua wazazi wake. Baadaye, mkewe mama Mkaja akafa. Mwenda alitoka kwao Reso na kuhamia mjini kwa mararu. Watoto walipomuona wakamrushia mawe wakimcheka na kumwita mwendawazimu. Akaishi maisha ya kuzururu watu wakiamini ni mwendawazimu isipokuwa rafikiye Mkwaya. Siraba alipotokea na kuelezwa haya yote, Mzee Josef akampeleka kwa Mwenda babake kupitia kwa Mkwaya.

3.2.2 Sentensi Fupi

Sentensi inaweza kuwa fupi ya maneno machache kama matatu mawili au hata moja mradi mwandishi ameeleza wazo lake kikamilifu. La muhimu ni kuwepo kwa kiima na kiarifu katika sentensi hiyo. Mohamed S. A. (1995:141) anasema kuwa sentensi fupi mara nyingi hutumiwa kujenga hisia za uchangamfu, harakati, woga, hofu au wasiwasi. Ufupi wa sentensi huzaa mapigo ya mizani mafupimafupi ambayo husababisha mwendo wa haraka katika mtiririko wa maelezo. Mtitimo wa harakaharaka pia ni zao la miinuko (mikazo au shadda) na mianguko(miregezo) ya sauti katika mtiririko wa silabi zake. Tunapoandika mfululizo wa sentensi fupi, huwa tunaweka makato miregezo, mipando na mishuko ya sauti yenye vipimo vya masafa mafupi na hili huleta mtitimiko wa haraka haraka ambao unakwenda sambamba na hisia inayojengwa. Sentensi fupi pia hutoa uanuwai na mabadiliko ya dhana mbalimbali. Mbali na mtitimo kuoana na maudhui, mizani inasaidia kujenga usambamba au urari wa matamko yanayotokea katika mfuutilizo wa vikundi, vishazi au sentensi.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ sentensi fupi zinabainisha hofu na wasiwasi wa msimulizi anapomwangalia Mfuko Mtupu. Tunasoma;

... na manywele yake timtimu,
na kutuzi lake lilo hanikiza, na
ramani ya mwili iliyomwota.
Alitisha. Aliogofya....
(uk.2).

Sentensi mbili fupi za mwisho zina takriri urari wa matamko. Silabi a-li zimerudiwa kwa mfululizo. Urari huu unaongeza mtitimo wa kasi unaoana na hisia za woga zinazojengwa na umbo la Mfuko Mtupu.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, tunasoma:

Halafu alitema mate, akakwang’ura
meno yake, kisha akatoa mlio wa
simba...“N’nakuuja siiimba.
N’takuua leo. N’takuua. Utakufa leo!”
(uk.26)

Maneno haya ya Daudi yanazua woga na wasiwasi. Kuna urari wa konsonanti ‘N’ unaopandisha tempo ya sentensi. Katika kutamka ‘N’takuua’, kuna mwiinuko wa sauti ambao unaleta mtitimo wa harakaharaka unaokwenda sambamba na hofu anayotaka kuzua msanii.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, maudhui ya hofu na woga yanasababishwa na mtitimo wa haraka wa sentensi hizi. Tunasoma:

Alicheka tena. “Wananyan’ganya.
Hawaziwezi nafsi zao. Hawaziwezi
njao zao. Hawauwezi unyonge wao.
Hawaukubali ufukara na uchochole.
(uk.110)

Mwenda anamlaumu mwizi anayemwibia mwanamke fulani mkoba wake na umati ukampiga hadi akamuua. Anapinga uozo wa wizi. Hizi sentensi fupi fupi zinaongezea kasi yake na usambamba wa viambishi ‘ha-wa’ vya ukanushi.

3.2.3 Nafasi ya Uakifishi Katika Sintaksia

Arege (2007:264) anasema kuwa kuakifisha ni kutumia au kutia alama kama vile nukta , koma, koloni, kiulizi, n.k. katika maandishi. Alama hizi hujulikana kama alama za uakifishi. Uakifishi ni utumiaji wa alama hizi ili kuzitenga sentensi, n.k. na hivyo kusaidia kuipambanua kwa uwazi maana katika tungo. Uakifishi ndio husaidia katika kuleta maana inayokusudiwa katika tungo. Matumizi mabaya ya alama za uakifishi huweza kupotosha maana inayokusudiwa au hata kuufanya ujumbe usieleweke. Kila alama ya uakifishi ina matumizi yake. Katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* mwandishi ametumia baadhi ya alama hizi za uakifishi kwa njia ya utokawaida. Matumizi haya yanabainisha ukiushi wake. Pia ametumia baadhi ya alama hizi kwa wingi katika hadithi zake.

Kwa mfano, msanii ametumia nukta tatu yaani (...) mahali kwingi katika diwani yake. Alama hizi huitwa alama za dukuduku.

Habwe na Matei (2006:124) wanaziita alama hizi ‘nukta za dukuduku’. Wanasema kuwa alama hizi hutumiwa kuonyesha habari fulani imeachwa kimakusudi. Mdokezo huu hutumiwa wakati mwandishi anataka kusema kitu fulani lakini anakidokeza kwa sababu fulani. Labda ni neno lisilo na upole au anataka msemaji mwenyewe ajalize. Nukta za dukuduku pia hutumiwa kuonyesha kukatizwa kwa usemi. Seti ya hivi vitone vitatu huonyesha kusita katika mazungumzo au maandishi yaliyokatwakatwa.

Katika Hadithi ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*, mbali na kwamba msanii ametumia alama za dukuduku kwa madhumuni haya, amezitumia kwa namna nyinginezo ambazo ni ukiushi. Kwanza ametumia alama za dukuduku kama alama za nukta.

Habwe na Nyonje (2007:26) wanasema nukta (.) ambayo wanaiita kituo inatumika kuashiria mwisho wa sentensi agizi na ya taarifa. Vile vile, hutumiwa katika uandishi na tarehe na nyakati. Wanaongezea kusema kuwa kituo kikuu wakati mwingine hutumiwa katika anwani za barua pepe na mtandao na hata kuakifisha vitabu vya marejeleo.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ , tunasoma:

‘Hata! Siondoki leo. Sibandui
mguu hapa na hapo. Nitakaa
kwenye kiti hiki. Nina haki
yangu hapa...’
(uk.4)

Badala ya kutumia kituo (.) mwishoni mwa usemi wa Mfuko Mtupu, Mohamed anatumia alama za dukuduku. Mwandishi anajenga taharuki kwa msomaji kutaka kujua sababu zinazompelekea mwenye mkahawa kumfukuza Mfuko Mtupu kutoka mkahawani baada ya Mfuko Mtupu kuvunja gilasi. Mfuko Mtupu anasema hatoki.

Kwingineko katika hadithi hii tunasoma:

“Sina ila unobe ambao umenifukuzia
mwanangu na kumfanya mke wangu...”
Alipofika hapo alisita na kumgeukia
mwenye mkahawa na mwenye mkahawa

hakuwa na makini tena... Nilianza kubaini
kitu na kutunga nia ya kukielewa. Ilinijia
tena dhamiri yangu ya kumsaidia mzee huyu.
Alipita tena yule mtumishi, nikamwita...
“Hebu, mletee mzee huyu pilau sahani moja...”
(uk.6).

Alama za dukuduku za kwanza baada ya ‘mke wangu’ zinatumiwa kwa usahihi. Kuna jambo ambalo halijasemwa ambalo mwandishi anataka tujijazie. Alama za dukuduku za pili baada ya ‘tena’ zinatumiwa kama alama ya kituo, kumalizia sentensi. Alama za dukuduku zinazotumiwa baada ya ‘nikamwita’ zinatumiwa kama kiakifishi koma (,) ambacho tutakirejelea baadaye. Alama za dukuduku za mwisho zinatumiwa kama kituo(.) kumalizia sentensi. Alama hizi zinamsaidia msimulizi kupata taswira kamili ya Mfuko Mtupu baada ya mkewe kuchukuliwa na mwenye mkahawa na mwanawe kupotea.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, tunasoma:

Na hapo nilikuona wewe bwana hakimu
ukiwana na Uledi na ulipomzidi
nguvu nilikushuhudia unamchoma kisu...”
(uk.143).

Mwandishi ametumia alama za dukuduku kukamilisha usemi wa Matwana mahakamani. Alama za usemi (”) zinaashiria mwisho wa sentensi. Alama hizi za dukuduku zinatumiwa kutia hamu wasomaji kutaka kujua hakimu alifanye nini kwa kunyoshewa kidole cha lawama na Matwana.

Baada ya alama ya kiulizi (?) na alama ya hisi (!) kutumiwa katika sentensi, alama nyingine haipaswi kufuata ila tu katika kuonyesha mtindo wa mwandishi. Katika hadithi ya ‘Hukumu’ tunaelezwa:

Je, akisema kweli, itanusuru roho
yake hii inayotaka kudhulumiwa?
Afanye nini? Ajinusuru vipi?...
Mawazo kila namna yalimparamia.
(uk.138).

Matwana anawana na nafsi yake ikiwa atasema ukweli mahakamani kuhusu muuaji wa Uledi au la. Alama hizi za dukuduku zinaongezea utata wake.

Kwingineko katika hadithi hii tunasoma:

‘na maiti yake ilionekana asubuhi
kwenye konde yangu, lakini hapana
shahidi aliyethibitisha hapa
kwamba mimi kaniona
nikinyanyua mkono wangu
kumchoma kisu Uledi rafiki
yangu!... Ilisadifu bwana
hakimu kwamba mimi nilikuwa
nikitoka msalani.
(uk.143).

Alama za dukuduku baada ya kivumishi ‘yangu’ kilichoweka alama ya hisi (!) hazifai. Zinachochea hisia za msomaji kujiuliza kama kweli Matwana alimuua rafiki yake Uledi.

Mohammed pia ametumia alama za dukuduku badala ya kutumia koma (,). Habwe na Nyonje (2007) wanasema kuwa koma hutumiwa kutenganisha maneno katika mfululizo wa orodha fulani, kutenga maelezo na kauli ya msemaji, kutenga swali na sentensi kuu na katika anwani. Pia hutumiwa kukiwa na sehemu inayovunja mtiririko wa sentensi, kuonyesha pumziko fupi katika sentensi na katika kuonyesha visehemu vya sentensi vinavyokinzana.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunasoma;

Na ghafla gilasi ikamponyoka
na kuanguka chini kwa mpasuko
mkubwa na kurusha vigae huku
na huko. “We, usijitie mwendawazimu
bure... utalipa hiyo gilasi. (uk.4)

Mwenye mkahawa anataka kumlipisha Mfuko Mtupu gilasi. Huku ni kumuongezea madhila. Alama za dukuduku zimechukua pahali pa koma kwani hajakamilisha usemi.

Aidha katika hadithi hii tunasoma;

N’na njaa ya kila siku ... n’na njaa ya
chakula, maji... (uk.6)

Alama za dukuduku zimechukua mahali pa koma kuelezea uchungu wa Mfuko Mtupu wa njaa mbalimbali alizonazo.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, tunasoma:

“Kesi nambari 16/7/82...
mshitakiwa Matwana Kusi”.
Msoma mashitaka alitangaza.
(uk.141)

Baada ya nambari ya kesi, kiakifishi mwafaka ni koma, si alama za dukuduku. Zinaonyesha kuwa maelezo ya kesi aliyonayo hayajakamilika.

Mohammed pia ametumia alama za dukuduku badala ya alama ya hisi(!). Arege(2007) anasema kuwa alama ya hisi hutumiwa kuonyesha mshangao katika kauli za kuamrisha au kuagiza na katika kuonyesha hisia nzito za kibinafsi. Pia hutumiwa kuonyesha kauli nzito katika dayolojia unapotokea msititizo wa neno.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunasoma;

Kila siku nikikwambia usije hapa husikii...
toka... toka... mwenye mkahawa alifoka
pale kaunta.
(uk. 4)

Neno ‘toka’ hapa ni amri na kawaida ingefuatwa na alama ya hisi. Alama hizi za dukuduku zinapunguza ukali wa mwenye mkahawa kwa Mfuko Mtupu kwani hata yeye mwenye mkahawa amemkosea Mfuko Mtupu, amemchukua mkewe.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, tunasoma:

Ko... ko... ko... hatua za viatu zilikaribia
mpaka pale mlangoni.
(uk.139).

Alama ya hisi ingefaa zaidi badala ya alama za dukuduku ili kusisitiza mlio wa buti za askari anayekaribia mlango wa Matwana mle jela.

Mtindo mwingine wa Mohammed ni kutumia kistari kifupi (-) katika baadhi ya sentensi zake.

Habwe na Matei (2006:121) wanasema kuwa kistari kifupi kina matumizi mbalimbali kama vile, kutenga silabi katika neno, kuonyesha silabi iliyoachwa kuendelezwa katika mstari unaofuata na kutenga kipindi cha wakati. Pia hutumiwa kutenganisha maneno ambatano na kuonyesha mzizi wa neno.

Mohamed ametumia kistari kwa namna yake. Tunasoma:

Jambo moja nilikuwa na hakika nalo.
Tofauti ya mimi na yeye haikuumbwa.
Ilibuniwa tu katika ulimwengu huu
wa mwenye-nguvu-mpishe.
(uk.3).

Msimulizi anapojilinganisha na Mfuko Mtupu, haoni tofauti. Ulimwengu tu ndio hubeba wenye nguvu na wanyonge kwa njia tofauti. Vistari hivi vifupi vimetumiwa ili kusisitiza nguvu za wenye mali wanaotawala ulimwengu.

Katika hadithi ya 'Pigo Kupokezana', tunasoma:

Huwaje yeye kumpa uzi wa roho

yake mtu mwingine au chezee?

Akija akiukaza je? Pamoja na

ujanja wake, hakujua vipi

Mtama - alijikuta tu anaghilibiwa.

(uk.22)

Mtama ana mawazo mengi kichwani akijiuliza ni vipi anamwacha mumewe awe anampiga na kumtusi kila siku kwa kipindi cha miaka saba. Kistari kifupi kinaonyesha kusita, kwa mawazo, kama koma akifikiria ni vipi anaghilibiwa.

Katika hadithi hii, bado tunasoma:

Kama ua, hupata siku chache za kuchanua

na kung'ara, na pale nyuki wanapolirukia

kulifyonza na kulitojezea unga wa uzazi,

halichukui tena hatua – hunyauka na

kukauka katika mapuuza ya mwanamme.

(uk.23)

Mwandishi katika kulinganisha maisha ya mwanamke na ya ua, anatumia kistari kifupi. Mwanamme (nyuki) anapomuuma, mwanamke hunyauka na kukauka. Kistari kifupi kinaeleza hali hii.

Penginepo katika hadithi hii tunaambiwa:

Juu ya ujanja wote huo, wenye bahati zao,
wajuzi wa kutega na kunasa, walimteka
Mtama. Haikujulikana yipi - mvulana
mmoja, Daudi kwa jina, kijana mzohali,
asiye mbele wala nyuma ila mwenye
heba, alithubutu kuupenya moyo wa Mtama.
(uk.24)

Mwandishi anatumia kistari kifupi ili kufafanua sifa za Daudi, kijana anayemnasa Mtama. Daudi ni mzembe na maskini. Watu hawatarajii kuwa angechaguliwa na Mtama. Kistari kifupi hakitangulizi ufafanuzi.

Katika hadithi hii, mwandishi pia ametumia kistari kifupi ili kufupisha nahau ‘akiwa amelewa chopi’ na pia kuonyesha hali ya ulevi wa Daudi kwa msisitizo zaidi katika maneno haya:

Siku hii kama kawaida ya Daudi
alirudi nyumbani kwake saa nane
za usiku _ chopi! Anayumbayumba.
(uk.25)

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, tunasoma:

Mwenda aliwaacha watu hao wawili
watokomee, naye aende na hamsini
zake – lakini kiasi cha kuwapa mgongo
tu, zilizuka sauti zilizoelekea kuja
upande ule ule wake.

(uk.109)

Kistari kifupi hapa kinatumiwa kama kipumuo kuonyesha mabadiliko ya mtiririko wa vitushi vya hadithi ya mwandishi. Mwenda anawaangalia hawa wawili, mwanamme na msichana na kuajabia mavazi yao. Halafu mwandishi anatoa mawazo huko kwa kutumia kistari kifupi. Matwana anasikia sauti kwingine.

3.2.4 Usambamba wa Kisintaksia

Msokile (1993:39) anasema kuwa usambamba ni matumizi ya maneno mawili au zaidi au fungu la maneno katika mfuatano maalum wa kisarufi. Vipashio vya kisintaksia vinarudiwarudiwa kwa utaratibu maalum katika tungo tofautitofauti . Urudiaji huu huzua mapigo ya aina moja yanayobainisha kwa uwazi kabisa linalolengwa na msanii.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, tunasoma:

Nilimjulisha na kumgundua ni mahuluku
aliyepagaa mwili. Jirimu lake upongoo,
na mararururu yake, na manywele yake
tintim, na kutuzi lake lilohanikiza, na
ramani ya mwili iliyomwota.

(uk.2).

Kuna urudiaji wa muundo wa kisintaksia unaodhihirika kwa matumizi ya maneno mawili mawili yaliyopigiwa mstari. Maneno haya yanafuatana kwa muundo wa nomino na kivumishi kimilikishi. Maneno haya yanamrejelea Mfuko Mtupu na kutupa taswira nzuri ya umbo lake.

Mfano mwingine wa mfuatano huu wa kisintaksia unapatikana katika maneno haya:

N'na njaa ya kila siku... n'na njaa ya chakula,
maji... N'na njaa ya mke wangu ambaye
bwana huyu muuza mkahawa ameninyang'anya.
(uk.6).

'N'na' ni kitenzi, 'njaa' ni nomino na 'ya' ni kihusishi. Mfuatano huu wa maneno kisintaksia unatilia mkazo njaa mbalimbali za Mfuko Mtupu, anaumia.

Katika hadithi ya 'Pigo Kupokezana', kuna maneno haya;

Nayo ardhi ya ujana ilikuwa pana
na huru kwenda alipotaka huku
akijigamba. Hakuna moyo wa
mwanamme usiotuturushwa na
umbo hili. Hakuna jicho la
barubaru lisilotaharukishwa na
uzuri huu!
(uk.23)

Sentensi mbili zilizopigiwa mstari zina urudiaji huu wa kisintaksia; kitenzi, nomino, kihusishi, nomino, kitenzi, kihusishi, nomino na kivumishi kiashiria. Mtama anajigamba kwa urembo wake alipokuwa kijana. Angeteka mwanamume yeyote aliyemtaka.

Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua', tunasoma:

Mambo mengi yamenivutia
Kwako huruma zako, ucheshi
wako, ukakamavu wako na
uhodari wako wa kazi.
(uk. 80)

Maneno yaliyopigiwa mstari ni mfuatano wa nomino na kivumishi kimilikishi. Maneno haya ni ya Mwanamaua akimwambia Dadi, mchumba wake. Mwanamaua anamsifia Dadi kwa maneno haya kabla ya kumsihi apigane na ng'ombe Kipelele ili adhihirishe ujasiri wake. Sifa hizi zinamchochea Dadi amkubalie Mwanamaua kinyume na matakwa yake. Sifa hizi zimetumiwa na mwandishi kufaulisha dhamira ya kichwa chake – ‘Mhanga wa Mwanamaua’ kwa sababu Dadi anakubali kupigana na hatimaye akuawa; anakuwa kafara.

Katika hadithi hii hii, tunasoma:

Kipelele alitolewa uwanjani.
Lenye vijipembe vidogo vya hadaa,
lakini lenye misuli iliyosimama
wazi mwili mzima. Linafoka.
Linatoka kipovu cha kinywa.
Limeinua masikio. Limesimamisha
mkia. Linaangaza mara huku
mara huku...
(uk.83)

Kiambishi ‘li’ kimekaririwa ili kuonyesha ukubwa wa Kipelele na kutayarisha wasomaji kutarajia kushindwa kwa Dadi. Matumizi haya yanaonyesha athari za kukubali kushawishika kwa Dadi kupigana na Kipelele kulikosababisha kifo chake.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, kuna mfano huu:

Kutoka hapo alimchuja yule mwanamke:

umbo lake, tambo lake, urefu wake na

mavazi yake ya kuchekesha ambayo

yeye bibi huyo angeyaita mavazi ya kisasa.

(uk.107)

Mvulana na msichana mmoja walimwita Mwenda mwendawazimu na mvulana kumwambia awapishe. Ndiposa Mwenda akaanza kuwakagua. Kuna mfuatano wa mchujo wa mwanamke uliojikita katika nomino na kivumishi kimilikishi kwa maneno yaliyopigiwa mstari. Urudiaji huu unammulika mwanamke huyu zaidi na kujenga taswira bainifu yake.

Kwingineko katika hadithi i hii tunasoma:

Wananyang’anya. Hawaziwezi nafsi zao.

Hawaziwezi njaa zao. Hawauwezi

unyonge wao, hawaukubali ufukara na

uchochole wao.

(uk. 110).

Usambamba wa kisintaksia unabainika kwa mfuatano wa vipashio hivi katika sentensi zilizopigiwa mstari; kitenzi, nomino na kivumishi kimilikishi. Urudiaji huu unatiliwa mkazo na silabi zilizofanana mwanzoni mwa kila sentensi – Hawa. Urudiaji huu unasisitiza ujumbe wa Mwenda wa kulaumu mwizi anayeiba na kupigwa hadi kufa.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, mwandishi anatumia usambamba wa kisintaksia wa mofimu fulani kutuonyesha athari za jinsi Mwenda anachukulia kuja kwa mwanawe Siraba, baada ya miaka ishirini huko Köln Ujerumani. Haonyeshi hisia zozote.

Tunasoma:

Mwenda hakujibu wala hakuonyesha kujali;
hakushangaa, hakushituka, hakufurahi,
hakununa, hakuinuka, hakusema kitu.
(uk. 119)

Mofimu 'ha-ku' zinatoa kwa uwazi kabisa hisia za Mwenda kwa Siraba mwanawe, zinatilia nguvu huzuni yake ya miaka mingi.

3.3 Ukiushi Katika Muundo wa Sentensi wa Kiima Kiarifu

Sentensi huwa kipashio huru kimuundo na kikubwa zaidi kati ya vile vipashio vya kiisimu ambavyo hutumiwa kisarufi. Vipashio hivi ni kama vile kategoria za maneno, virai na vishazi. Obuchi na Mukhwana (2010:173) wanasema kuwa kimsingi, kishazi ni sharti kiwe na muundo wa kiima na kiarifu.

Tuki (1990) wanaifafanua dhana ya kirai kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini kisichokuwa na muundo wa kiima kiarifu. Kama tulivyokwishasema, kiima hueleza yule anayetenda au anayehusika na kitendo fulani. Kwa kawaida, kiima ni lazima kiwe na nomino au kiwakilishi chake katika sentensi. Sentensi yoyote haikamiliki pasina kiima.

Kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo aghalabu hufahamisha kuhusu kitendo kinachotekelezwa na nomino au kiima. Kiarifa hutaja jambo linalofanywa na kiima au linalofanyiwa kiima. Kwa sababu hiyo, neno kuu katika kiarifa huwa ni kitenzi kama wanavyosema Obuchi na Mukhwana (2010:173). Kuna uwezekano wa kiarifu kusimama pekee pasina kiima. Sentensi kamili ya Kiswahili hubeba muundo wa kiima kiarifu. Bila sehemu mojawapo, inakuwa ni ukiushi wa kimtindo. Mohamed anasawiri baadhi ya sentensi zake bila mpangilio huu wa kiima kiarifu.

Katika hadithi ya 'Mfuko Mtupu', tunasoma:

Kila kitu cha mzee huyu kimechukua
taathira kubwa juu yangu. Ujaji wake
na kukaa kwenye kiti mbele yangu.

Mwili wake. Mchukuo wake.

Wasifu wake. Hali yake. Yote
yalikuwa kama mkusanyo wa
shehena ulionilemea kwa hisia
nzito.

(uk.1)

Sentensi nne zilizopigiwa mstari hazina kitenzi, sehemu ya kiarifu. Zina sehemu ya kiima tu. Sehemu hizi zimeundwa kwa nomino na kivumishi kimilikishi. Huu ni ukiushi wa kimtindo unaoelezea wasifu wa Mfuko Mtupu zaidi. Kuja kwake na sura yake ni mambo yanayomwathiri msimulizi. Ni taswira ya shida.

Katika hadithi hii, tunasoma tena:

Alitoka nje huku akicheka na
kuuacha ukumbi wa mkahawa
baridi. Watu wote walitumbua
macho. Wengine tonge mkononi,
wengine chakula kinywani.

Sikuweza kukaa tena.

(uk.7)

Baada ya Mfuko Mtupu kukataa kununuliwa chakula na msimulizi, anatoka nje ya mkahawa na kuwaacha watu wameduwaa. Wengine tonge mkononi, wengine chakula kinywani ni muundo wa kiima tu wa kiwakilishi, nomino na kielezi. Hamna kitenzi.

Katika hadithi ya ‘Tumbo Iliyovia’, tunasoma:

Saada hakujibu kitu.
Alivundumka, akafutuka,
akatimka na Miraji akafuata
nyuma akinasihi na kumbembeleza.
Usiku huohuo.
(uk.35).

Saada anapowasili kwao Bumbwisudi baada ya miaka mitano Ulaya, wazazi na wanakijiji wanashuhudia mabadiliko makuu. Hakuna anayemsalimia hata wazazi wake, anakataa chakula chao na hata kukataa kulala kwa nyumba ya wazazi wake. Miraji aliyekuwa rafikiye kabla ya kwenda Ulaya anataka kujua shida yake. Saada hamjibu na badala yake anaondoka. Usiku huohuo ni nomino na kisisitizi bila kitenzi ili kuonyesha mkengeuko wa Saada unaomsukuma kuondoka kwao usiku huohuo anaofika bila kusubiri asubuhi.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia,’ tunasoma:

Si mahuluku wa makosa?
Uwongo, uwongo ... Aljiambia
moyoni wake.
(uk.55)

Haya ni mawazo ya Kassim baada ya kukosolewa na Sheikh Majid kuhusu ulevi wake na kukimbizana na mabinti. Kassim anajiuliza kwa nini ni vijana tu husingiziwa na siyo mashehe wa dini? Sentensi ‘uwongo, uwongo’ haijakamilika kwa maana haina kitenzi. Inatilia nguvu maudhui ya unafiki wa mashehe unaojitokeza baadaye na kuwamulika kama waongo kwelikweli. Nukta tatu zinazotumiwa badala ya koma zinaashiria kuwa kuna zaidi ya yasemwayo, na kweli yapo.

Katika hadithi ya ‘Mhanga na Mwanamaua’, tunasoma:

Hakubali wala hatulii mpaka
afanikiwe au labda patolewe
mhanga au chano. Usiku mmoja
wa machumi ya karafuu. Usiku
ulioshiba kiza kinene.
(uk. 76)

Mwanamaua anatoka kwao nyumbani bila kumwambia yeyote ili akakutane na Dadi, mchumba wake. Sentensi iliyopigiwa mstari inasisitiza kuwa ulikuwa ni usiku, wakati wa kuchuma karufuu. Sentensi hii haina kitenzi ili kusisitiza umuhimu wa usiku huu. Mwanamaua anafaulu kumshawishi Dadi apigane na ng’ombe Kipelele kinyume na kupenda kwake; ulikuwa usiku wao wa mwisho maana anauawa siku inayofuata na ng’ombe huyu.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, tunaeleza:

Alitazama juu. Huko kuna nini? Mbingu, mawingu
na pengine jua. Na usiku? Usiku mbingu, nyota na
mwezi. Nani kaviumba vitu hivi? ... Yu wapi Bwana
Mungu? Alipiga kelele. Halafu akasita ghafla.
Akatweta. Pumzi mbili mbili.
(uk.112).

Mwenda anaangalia juu na kuanza kufikiria kuhusu nani kaumba mbingu, mawingu, jua, usiku, mwezi na nyota. Sehemu hii imekaliwa na kiima tu bila kiarifu.

Jazba zinapopanda, anatweta na kupumua kwa nguvu, pumzi mbili mbili pia hamna kitenzi.

Tena tunaambiwa:

Mititigo na mingurumo ya gari,
honda, viskuta, marikwama, honi,
kengele za baiskeli mfululizo.
Pitapita. Nenda rudi. Mradi zogo.
Mwenda hakuwa na pahala maalum
pa kwenda.
(uk.112)

Katika kutilia nguvu fujo ya mjini , mwandishi anaandika mradi zogo bila kiarifu kusisitiza vurugu hii. Huu ni mtindo wake unaombainisha.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, tunaelezwa:

Alionekana kutia chumvi
katika kila kitu, rangi ya
mdomo, podari, kujirashia
mafuta mazuri, kuzikoleza
kope wanja, kuifuata mistari
miembamba ya nyusi zake
kwa penseli maalum. Alitia
chumvi toka miondoko hata
minyanyuko. Kila kitu, kila
hatua... Fumu alijua fika
kwamba taa ya mapenzi na
Naima isingeyumkinika.

(uk.131)

‘Kila kitu, kila hatua...’ ni sentensi isiyo na muundo wa kiim kiarifu kwa sababu imekosa kitenzi. Nukuu hii inaweka wazi mapambo anayofanya Naima kabla ya kwenda kwa Bi. Kitimbi ili asikataliwe. Angekataliwa huko, mipango yake ya kumuaibisha mumewe Fumu na kufichua uasherati wake ingetumbukia nyongo.

3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeanza kwa kufafanua maana ya sintaksia. Tumesema ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyingine zinazoiunda.

Baada ya kufafanua dhana hizo, tumejadili kwa mapana ukiushi wa vipashio mbalimbali katika sentensi. Viapashio ambavyo tumeviangazia ni: nomino, vielezi, viunganishi, vihusishi na

vivumishi. Tumetoa mifano anuwai ya ukiushi wavyo, sababu za ukiushi huo na kutoa maoni yetu vile sentensi hizi zingeandikwa katika hali ya kawaida.

Mbali na hayo, tumegusia sentensi ndefu na fupi katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumetoa mifano ya sentensi hizi huku tukionyesha majukumu na athari yazo katika diwani hii.

Fauka ya hayo, tumeangazia nafasi ya uakifishaji katika sintaksia ya diwani hii.

Tumeonyesha alama za uakifishi alizotumia kwa utokawaida kwa wingi. Alama hizi ni kama alama za dukuduku na kistari kifupi. Tumetoa sababu za kuzitumia pamoja na athari zake katika sentensi.

Isitoshe, tumeangazia usambamba wa kisintaksia katika kazi hii. Tumetoa mifano kadhaa pamoja na kuonyesha athari zake katika uelewekaji wa sentensi.

Mwisho tumemulika ukiushi wa kutozingatia muundo wa sentensi wa kiima kiarifu. Tumetoa mifano ya ukiushi huu na majukumu yake katika muktadha wake.

Katika sura ya nne inayofuata, tumechanganua ukiushi wa kisemantiki.

SURA YA NNE

UKIUSHI WA KISEMANTIKI KATIKA *MFUKO MTUPU NA HADITHI NYINGINE*

4.0 Utangulizi

Semantiki ni tawi la isimu linalochunguza na kuchambua maana za maneno au sentensi katika lugha. Massamba (2004: 75) anaiita semantiki ‘Elimumaana’. Lugha ina vipashio kadhaa vinavyomwezesha mwandishi kuchagua vile anavyotaka kwa dhamira ya kujieleza ipasavyo.

Said A. Mohamed ametumia lugha inayovutia kisanaa ili kuwasiliana na hadhira yake. Katika sura hii, tumeshughulikia jinsi mwandishi amekiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuzua maana mbalimbali katika kazi yake. Tumeonyesha jinsi ukiushi huu unatilia nguvu maudhui yake na kuimarisha uelewaji wa msomaji wa diwani hii. Tumejadili tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha kama vile takriri, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi, usambamba wa visawe, jazanda, methali, barua na nyimbo. Mbinu hizi zina uhusiano na semantiki kwa maana zinabeba maana mbalimbali katika muktadha zinamotumiwa.

4.1 Tamathali za Usemi

Kwa mujibu wa Msokile (1993: 39), tamathali za usemi ni maneno, nahau au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi hayo. Anaongezea kusema kuwa tamathali za usemi zinatumiwa pia kupamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha.

Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979: 32), tamathali za usemi ni viwakilisho au vifananisho vya dhana nyingine tofauti au zilizofanana. Wamitila (2008 :393)anaeleza kuwa

lugha ya kitamathali ina majukumu matatu makuu; (a) Urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa na lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa au kiumbuji, (b) Ufafanaji au uelezeaji wa kinachohusishwa na tamathali maalum na (c) Uthabitishaji, yaani kukifanya kinachorejelewa kuwa na uthabiti fulani, na kwa njia hii, mkokotezo mkubwa.

Kwa hivyo, tamathali za usemi ni kifungu cha maneno kinachotumiwa kupanua au kubadilisha maana ya wazi au ya kimsingi na kukifanya kuwa na maana nyingine tofauti. Lugha hii inayotumiwa kwa ubunifu mkubwa huboresha kazi ya mwandishi na kuifanya inate na kuwa na mvuto mkuu. Mifano ya tamathali za semi ambazo tumechunguza ni tashbihi, sitiari, kinaya, tashhisi, tanakuzi, majazi, tasifida, maswali ya balagha na chuku.

4.1.1 Tashbihi

Neno ‘tashbihi’ limetokana na neno ‘shabihi’ ambayo ina maana ya kufanana au kulingana na kuwa sawasawa. Kuhenga (1977:4) anasema kuwa tashibiha (kama anavyoiita) ni mtindo wa uneni wa kifani, ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au hufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti, kuwa na ufanano au ushabibiano fulani fulani wa hali ya utendaji au maumbile, mathalani, sura, rangi na jinsi ya kujimudu. Kwa kawaida, tashbihi huonyeshwa kwa kutumia maneno kama; mfano wa, mithili ya, vile na sawasawa. Tashbihi hubainisha mpaka bayana wa ulinganisho na pia kuonyesha wazi jinsi ulinganisho huo ulivyo. Haya ni kwa mujibu wa Leech (1969: 156). Ulinganisho huu wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa tofauti hubainisha maana kwa njia iliyo wazi kabisa.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ msimulizi anataka kumuagizia Mfuko Mtupu sahani ya pilau anayeonekana mwenye njaa. Kwa kuonyesha maudhui ya bidii katika madhari ya mkahawa huu, mtumishi hakamuona. Tunaelezwa:

Sifikiri kama nilizua taathira
yoyote kwa yule mtumishi
niliyeanza kumwashiria na
ambaye alinipita kama
wimbi la upepo
(uk.1)

Kifananisho ‘kama’ kinatambulisha tashbihi hii na kuonyesha shughuli nyingi katika mkahawa huu.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, Mtama hana nguvu za kumpinga mumewe Daudi. Anakubali matusi na vipigo vyake bila kujitetea. Tunasoma:

alijitia kuvutana nazo nguvu
zisizoonekana, zilizomtuma
kukubali kufuata kama
gombe lililotiwa shemere
(uk. 22)

Shemere ni kamba anayofungwa ng’ombe puani ili kudhibitiwa. Mtama anasabilia maisha yake avutwe kama ng’ombe bila pingamizi yoyote. Tashbihi hii inaonyesha maudhui ya nafasi ya mwanamke katika jamii asiye na sauti ya kujitetea.

Aidha; katika hadithi hii, tunaelezwa;

wale watoto wao wawili
kama macho, Zamda na Riziki
(uk. 24)

Daudi anashindwa na jukumu lake la kumlisha mkewe na watoto. Inabidi Mtama ajikaze kwa kila namna awatafutie mabinti wao wawili chakula. Mwandishi analinganisha idadi ya watoto hawa wawili na macho mawili ya mtu. Tashbihi hii inaacha athari kuu kwenye sikio la msomaji.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, baada ya Saada kwenda Ulaya kusomea uwakili alirejea kwao Bumbwisudi akiwa amebadilisha nywele zake, mavazi yake na uso wake. Mwandishi anasema:

Uso wake mweusi sasa ulikuwa
mweupe kama shetani
(uk.32)

Kwa kawaida, shetani uhusishwa na weusi, rangi ya giza na uovu na sio weupe unaohusika na uzuri. Huu ni ukiushi na uteuzi wa kipekee wa Said Ahmed. Saada kuwa mweupe kama shetani ni tashbihi inayotilia mkazo maudhui ya kugeuka kwake anapobadilisha siyo tu mavazi na nywele lakini uso wake pia.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Sheikh Majid anashutumu Kassim kwa ulevi wake na kukimbizana na wasichana. Kassim anajua unafiki wa Sheikh na kumwekea mtego ili wakutane forodhani huku akijifanya ndiye Maryam. Kwa siku nyingi, Sheikh alimtaka Maryam bila mafanikio. Kabla wakutane, tunaambiwa:

Sheikh Majid aliona jinsi
mkono wa Bi.Maryam ulivyokuwa
ukipungwa. Kama fisi, aliumezea mate.
(uk. 59)

Fisi uhusishwa na tamaa iliyokithiri ya vyakula. Tamaa ya Sheikh ya kumtia mikononi mwake Maryam ilikuwa kubwa kama ya fisi. Tashbihi hii inatilia mkazo maudhui ya tamaa ya mwili na inapokuwa ni ya Sheikh, kiongozi wa dini, ni unafiki mkuu. Tashbihi hii inachangia pakubwa katika uelewekaji wa maudhui haya.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda anaeleza mavazi ya vijana wawili anaokutana nao wakamwita mwendawazimu. Tunaeleza kuwa:

wote walikuwa wamevaa
miwani kubwa za jua
zenye vioo vya duara vikubwa
kama visahani vya chai
(uk. 109)

Tashbihi hii inatilia msisitizo ukubwa wa miwani ya vijana hawa na kuonyesha ubunifu mkuu wa mwandishi katika kujenga picha mwafaka katika akili za wasomaji.

Kwingineko katika hadithi hii tunaeleza kwamba Mwenda aliuza ng’ombe na shamba lake ili ampeleke mwanawe Siraba ng’ambo akasome. Siraba hakurudi wala kuwasiliana naye. Baadaye, mkewe anapoaga, Mwenda anachukulia kujitolea kwake kwote kama kazi bure. Kwake,

yote aliyofanya yalikuwa
kama kutia magunia ya
sukari baharini!
(uk. 117)

Mtu anapotia magunia ya sukari baharini, ni kazi bure kwa maana hawezi akaikoleza utamu yote. Tashbihi hii inamulika majuto ya Mwenda kwa mwanawe na pia uchechefe wa shukrani wa Siraba kwa babake.

Aidha, katika hadithi hii tunasoma:

uso wake ulitazama *kama*
zuzu; kama mwendawazimu.
Alibaki kama jiwe lisilokuwa
na hisia yoyote
(uk. 119)

Tashbihi hizi zinamrejelea Mwenda baada ya mwanawe Siraba kurudi kutoka Ujerumani. Anarudi baada ya miaka ishirini. Mwenda hana hisia zozote kwake (mwanawe) ni kama jiwe kwani hamjali. Tashbihi hizi zinaonyesha wazi athari za unyama wa Siraba wa kusahau wazazi wake alipoenda ng'ambo.

Katika hadithi ya 'Njia Fupi', usaliti wa Fumu kwa mkewe Naima unafichuliwa. Anazoea kutembelea mahawara katika nyumba ya Mama Kitimbi. Mkewe Naima anapomfumania, tunasoma:

Fumu alijiona yumo katika
ndoto. Aliduwaa, akaganda
kama sanamu.
(uk.135)

Tashbihi hii inatilia mkazo maudhui ya usaliti wa Fumu. Sanamu ni jiwe na haliwezi kusonga. Aibu ya Fumu ya kumlemeza viungo vyake asiweze kusonga inafananishwa na sanamu na kuchangia pakuu uelewa wa hali yake.

4.1.2 Sitiari

Mohamed (1995) anakariri kuwa kwa sababu neno sitiari lina vijezezi vingi, yeye atatoa vigezo mbali mbali vinavyotumika kuamua kama neno limetumika kisitiari au la, na kuonyesha kiasi gani waandishi wa nathari ya Kiswahili huvitumia vigezo hivyo kuundia sitiari zao. Kigezo cha kwanza ni kuwa sitiari ni chombo cha ubinafsi kinachotumiwa kuelezea ulimwengu wetu wa ndani na nje kwa kuyagawa mazingira yake na kuyaweka katika dhana mbalimbali kama ndio maarifa yetu. Kigezo cha pili ni cha uhusisho kati ya kitajwa (dhana) na muundo (umbo) la lugha. Kwa kuwa uhusiano huu si wa kimaumbile, hakuna sababu yoyote ya kumzuia mtu shujaa kutoitwa simba badala ya shujaa. Kigezo cha tatu ni uwezo wa sitiari wa kufumbata dhana pana kwa neno moja au maneno machache kwa kutumia picha. Nne ni sitiari nyingi zina sifa za upya usiozoeleka. Upya huu unazifanya ziwe imara na zenye kushawishi vizuri kisanaa na kumvutia msomaji.

Mohamed anamalizia kwa kusema kuwa, katika kuunda sitiari, vitu viwili vinawekwa sambamba katika ulinganifu na kutumia sifa au tabia za aina moja. Kwa kawaida, vitu vinavyolinganishwa ni tofauti sana lakini hatimaye vinachangiana sifa au tabia moja.

Massamba (2004:83) anafafanua sitiari kama namna ya usemaji ambapo kitu hupewa jina la kitu kingine kwa namna ya kukipa uzito au kukitilia mweka kile kilemwacho. Kulingana na Wamitila (2008) na Kuhenga (1977, sitiari haitumii maneno ya mlinganisho kama ‘mfano wa,’ ‘tamthili ya,’ ‘kama,’ ‘ja’ na ‘kama vile’.

Leech (1969: 151) anasema kuwa sitiari imehusishwa na sheria mahususi ya uhamisho inayosema ‘F = ni kama L’. Maana yake ni kuwa ‘F’ ina tabia au sifa kama ‘L’. Ingawa ‘F’ na ‘L’ ni vitu viwili, tofauti, huwa kuna uhusiano fulani kati yavyo unaovifanya vihusishwe. Kwa

hivyo, sitiari hulipa neno au dhana jina la kitu kingine bila kutumia vilinganishi vyovyote. Sitiari huficha na kusitiri maana ya jambo kwa ufananisho wake usio bayana.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, msimulizi anapomwagizia Mfuko Mtupu sahani ya pilau, Mfuko Mtupu aliyekuwa amekaa anavuta kiti nyuma na ghafla anakamata meza na kuisukuma na kuporomosha vyote vilivyokuwa juu yake. Ghafla anamrukia msimulizi na kumshika ukosi wa shati na kumwambia hakutaka chakula wala pesa zake. Halafu anamuachilia na kuanza kulia na kusema ana njaa ya kila kitu. Baada ya kusema hakuna anayemwamini katika jamii yake, anatoka ghafla nje huku akicheka. Wateja wa mkahawa wanashuhudia haya yote na baada ya kutoka, tunaelezwa aliuacha ukumbi wa mkahawa *baridi*. Watu wote wanatumbua macho. (uk. 7). Neno ‘baridi’ ni sitiari kwa maana ya kimya au kutulia bila kelele. Ubaridi umelinganishwa na ukimya ili kubainisha wazi athari za maneno na matendo ya Mfuko Mtupu anayefikiria kuwa jamii ilikuwa imemnyanyasa.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, mwandishi anasema:

Mtama alikuwa Mtama
Kweli! Wacha ndege warukeruke
na kutua nyumbani
kwao.
(uk. 23)

Mwandishi anamlinganisha mhusika Mtama na nafaka ya mtama. Ndege ni wanaume waliokuwa wakienda kwao kumchumbia. Sitiari hizi zinabainisha wazi maudhui ya uchumba na hekaheka za wanaume vijana kuwatafuta wenza wao wa maisha.

Penginepo katika hadithi hii tunaelezwa kuwa Daudi, mumewe Mtama anamsimanga Mtama, na kumpiga magumi ya bure kila siku. Kwa Daudi, tunaelezwa:

Kwake ndoa ilikuwa namna
moja tu: kupata mwanamke
wa kumdhibiti na kumgeuza
gombe la gari
(uk. 24)

Daudi anamfanya Mtama kuwa kama ng'ombe anayesukuma gari bila kulalamika. Sitiari hii inaonyesha maudhui ya taasubi ya kiume ambapo mwanaume hujiona bora kuliko mwanamke na humuona kama chombo kisicho na sauti. Dhana hii inatiliwa mkazo na Mtama ambaye tunaelezwa 'akajiachia achomwe mikuki ndani ya moyo wake'. (uk. 24). 'Mikuki' ni mateso anayopata na yaliyokuwa machungu. Pengine katika hadithi hii tunaelezwa:

akaogofya kama paa
kwenye situ lenye
simba. Sura ya Daudi,
shetani au mtu alikuwa
na uchawi fulani kwake.
(uk. 24-25)

Mwandishi anamrejelea Daudi kama simba na shetani kutokana na vitendo vyake vya kikatili kwa mkewe. Daudi na simba au shetani hawana tofauti. Uchawi ni mizungu ya Daudi inayomteka Mtama. Sitiari hizi zinaibua hisia za kinyaa kwake kutoka kwa wasomaji.

Katika hadithi ya 'Tumba Iliyovia', watu wa Bumbwisudi wanajivunia Saada, mzaliwa wa kijiji chao 'aliyekwenda kubeba uchawi na wazungu huko ulaya'. (uk. 30).

‘Uchawi’ ni nguvu inayoaminiwa kubadilisha mazingira kwa uzuri au ubaya. ‘Uchawi’ ni sitiari ya ‘ujuzi’ au ‘utaalamu’ ambao Wanabumbwisudi wanaamini Saada angeutoa Ulaya ili kuleta mabadiliko katika kijiji chao, angewafaa kwa uwakili wake. Sitiari hii inatilia mkazo jinsi elimu ya nje kama Ulaya hupewa hadhi kuu na Waafrika. Tena, inatueleweshwa zaidi matamano ya wanakijiji waliokuwa nayo kwa Saada.

Aidha, katika hadithi hii, Miraji, aliyekuwa rafikiye Saada kabla hajaenda Ulaya anamshauri na kumkosa Saada. Saada anampuza Miraji, anakataa chakula anachopikiwa na mamake Bi.Mhando na hata kukataa kuwasabahi wanakijiji wake. Anamwambia:

Umekuwa kama mkekewa
husafiriki kwa miba. Kumbuka
Saada, hukuwa hivi. Ulikuwa
waridi lisilo miba katika
mbolea halisi iloyokulea. Lini
utarejea kwenu?
(uk. 35)

Miraji anatumia sitiari kumkumbusha Saada kuwa zamani alikuwa waridi na sifa mojawapo yake ni ua linalonukia vizuri. Hakuwa mwenye miba kwa maana ya mapuza, masimango na hata matusi yake anayowafanyia wazazi na wanakijiji. ‘Mbolea’ ni sitiari ya mazingira ya Bumbwisudi anakokulia kwa kufunzwa tabia stahiki. Sitiari hizi ni miongoni mwa ithibati zinazotambulisha usanii wa mwandishi katika kuyapa maneno yake uhai ili kuibua picha halisi ya kuongoza uelewa wa watu.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Kassim anajiuliza:

Kwa nini, alijiuliza, hujuma
zote za namna hii ziwazukie
wao vijana na wasiokuwa
miamba ya dini?
(uk. 55)

‘Mwamba’ ni jabali lililoko baharini chini ya maji au nchi kavu. Katika sitiari hii, Kassim anajiuliza kwa nini vijana hawawezi wakawa majabali ya kuweza kustahimili vishawishi vya ujana. Miamba pia inarejelea viongozi wa dini ambao anawachukulia kuwa ni wenye nguvu za kustahimilia dhoruba kali za dunia.

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’, Mwanamaua anatoka nyumbani kwao usiku kwenda kukutana na Dadi, mchumba wake. Yeye anakifurahia kile ‘kiza kwa sababu ni kiza, *buibui* kubwa la wezi na wahalifu’. ‘Buibui’, sitiari ya kiza ina maana ya ‘nguo aghalabu nyeusi ambayo huvaliwa juu ya nguo nyingine na wanawake haswa wa kislamu kulingana na *Kamusi ya karne ya 21*’ (2011). Buibui hufunika nguo ya ndani na hapa kiza ni siri kati ya Mwanamaua na Dadi. Sitiari hii inatilia mkazo maudhui ya papara za wachumba walio tayari kufanya ya hatari mradi wakinaishe tamaa zao.

Baadaye katika hadithi, baada ya Dadi kupigana na ng’ombe Kipelele na kuuawa, ‘kwa nukta chache uwanja ulikuwa *baridi*’. (uk. 85). Baridi ni sitiari ya ‘kimya’, hali inayowavaa washangiliaji wa mchezo huu. Hofu na mshituko unawaingia wote na wananyamaza. Huu ni mtindo wa mwandishi wa kueleza ‘ukimya’ maana ametumia sitiari hii katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’. ‘Baridi’ hapa inatupa taswira halisi ya watazamaji wa mchezo wa ng’ombe na mtu na jinsi wanavyoathirika baada ya Kipelele kumpiga mapindi Dadi na hatimaye kunyooka.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, Matwana anahofia hatima ya kesi yake. Amekamatwa na kushtakiwa kwa kumuua Uledi. Hofu yake inatokana na ukweli kuwa muuaji halisi alikuwa hakimu anayesikiliza kesi yake. Tunaeleza:

Alishindwa kwa sababu fikra
ya kwamba muuaji alikuwa ni
mmojawapo wa wale wenye
funguo za kuliendesha lile
sanamu.
(uk. 138)

‘Funguo’ ni sitiari ya ‘nyenzo’ au ‘njia za’ ilhali ‘sanamu ni ‘kesi yake’. Kwa kawaida sanamu huwa haisongi kwa maana ni jiwe. Kwa Matwana, kesi yake ni gumu kuitatua na kumpa haki anayostahili. Sitiari hii inaonyesha unafiki wa jaji aliyetekeleza mauaji na kumsingizia maskini Matwana.

4.1.3 Kinaya

Mbatiah (2001) anasema kuwa kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile unachosema. Kinaya huangaza utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo sasa.

Kuna wataalamu kama Wamitila (2008) wanaochukulia kuwa kinaya ni sawa na kejeli. Kuhenga (1977) naye anasema kuwa kejeli ni uneni wa kimafumbo ambao humuudhi mtu kwa nia ya kumuonya kichinichini bila ya bughudha. Mbatiah (2001) anakubaliana na maana hizi kwa kusema kuwa kejeli au kijembe ni matamshi yanayolengwa mtu ili kumtweza kwa sababu huwa ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Mtu anapopewa sifa ambazo hazistahili, basi huwa anakejeliwa au kupigwa kijembe. Anaendelea kusema kuwa ingawa kejeli huchukuliwa kuwa

kisawe cha kinaya, inafaa kusisitiza kuwa kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee. Kinaya basi ni usemi unaokusudiwa kutoa maana kinyume na kinachosemwa kwa ajili ya kuonya, kumshutmu au kutweza mtu.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, ni kinaya kwa mhusika Mfuko Mtupu kukataa kununuliwa chakula na msimulizi ilhali anasema ana njaa ya kila kitu; chakula, maji, na mke wake. Ni kinyume cha mambo anapokiri:

Nani kakwambia kwamba
nina njaa? Nani ahh! Mimi
sina njaa na wali wenu
wala fedha zenu. Mimi
nina fedha tele ninazowadai
hawa.
(uk.6)

Majivuno ya Mfuko Mtupu yanatilia mkazo kinaya hiki maana anasema:

Mimi usinione hivi kijana,
nimekuwa mwalimu wa kila
mtu hapa. Nilianza kusomesha
toka miaka ya arobaini na
saba na leo nimeishia kuwa nani?
(uk. 6)

Mwandishi anatumia Mfuko Mtupu kuwakejeli wafanyikazi ambao hawana kitu, hata cha kujinunulia chakula baada ya miaka mingi kazini.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, Mtama anachumbiwa na wanaume wengi wanaomtaka. Wanamtafuta kwao na mjini, anapita akijitupa na kujivunia ujana wake. Anawakataa

‘waungwana wenye majina yao’(uk.23) kwani anatumia ujanja kuwaepuka wote. Ni kinyume cha matarajio kwa Mtama anapolewa na Daudi. Mwandishi anasema:

Juu ya ujanja wote huo,
wenye bahati zao, wajuzi
wa kutega na kunasa,
walimteka Mtama.
Haikujulikana vipi-mvulana
mmoja, Daudi kwa jina,
kijana mzohali, asiye mbele
wala nyuma, ila mwenye
heba, alithubutu kuupenya
moyo wa Mtama.
(uk. 24)

Mwandishi anamkebehi Mtama kwa kumchagua Daudi ambaye hangeweza kuilisha familia yake pamoja na dhila la kumpiga kila siku. Kinaya hiki kinaonya vijana kuchagua kwa uangalifu wachumba wao wa ndoa.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, Bwana Haji na Bi. Mhando wanapanga mipango kabambe ya kumpokea bintiye Saada kutoka Ulaya. Maandalizi yanahusu vyakula murua, usafi wa nyumba na hata kuwaalika wageni kufika kwao kumpokea binti yao. Saada anapowasili kwao, matukio yalikuwa kinyume cha matarajio. Hawasalamii wazazi wala wageni mbali anasema:

Kundi lote lile limekuja kufanyaje?
(Alimwambia mamake)
Mimi si mtume, kama wamekuja
kupokea baraka zangu, wala si
waziri kama naweza kuwaahidi
kujenga shule Bumbwisudi,

aliendelea kwa sauti yenye kiimbo
cha kizungu.
(uk. 33)

Badala ya kufurahia mapokezi, Saada anawakaripia wanakijiji kwa maringo akifikiri walitaka msaada wake sana. Kinaya kinatumiwa kubeza kupapia tamaduni za kigeni zinazoumbua mtu na kumfanya ‘mgeni’ kwa watu wake. Mwandishi anasuta tabia hizi.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Sheikh Masoud anamuonya Kassim dhidi ya ulevi na usherati. Baada ya haya, tunasoma:

Kassim alicheka tena moyoni.
Moyoni alisema maneno ya
kukebehi. Moto wa dunia na
ahera hauwaunguzi mashehe.
Dunia haiwadamirishi wacha
Mungu. Hawa watu wenye
vifutio vyao...
(uk. 56)

Sheikh Masoud ni mnafiki anayejificha nyuma ya dini kutenda uasherati wake. Anavaa ‘miwani ya jua’ (uk.58) usiku saa tatu akienda kukutana na Maryam ili afiche unafiki wake. Mwandishi anashutumu unafiki wa watu wasemao ni wacha Mungu kumbe ni fisi. Kusema moto wa ahera si wao na Mungu kutumia vifutio maalum kusahihisha makosa yao ni kinaya kikubwa.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, mwandishi anasimulia kisa cha kijana mmoja anayempokonya mwanamke kibeti chake. Raia wanamfukuza na wanapomkamata,

anapigwa mateke, magumi, viatu, fimbo, mawe, matofali hadi akafa. Mwenda aliyeshuhudia unyama huu tunaelezwa alijisemea:

Mwenda aliwatazama wale watu
waliokuwa wakitawanyika baada
ya tukio hilo. Bila ya
shaka walikuwa wamefurahi.
Wametosheka kujifua na kupunguza
kani zao za ndani kwa ndani
(uk. 110)

Ni kinyume cha mambo watu kufurahia baada ya kumuua mtu hata kama ni mwizi. Kumuua mtu ni kilele cha ukatili wa kibinadamu. Kule kufurahia kufa kwa kijana huyu ni kukejeli unyama wa mtu ambaye hayaoni makosa yake mwenyewe.

Wamitila (2008) anasema kuwa kicheko na urefushaji wa silabi ni mbinu zinazotumiwa sana hasa katika drama kuashiria kinaya. Kwa misingi hii, hadithi hii ina vicheko vingi. Vicheko vya Mwenda vinaashiria maana kinyume. Baada ya Mwenda kushuhudia kupigwa kitutu kwa mwizi kijana katika maelezo ya awali, Mwenda anacheka. Tunaambiwa:

Wanaibaaaaaaaaaaaa. Wananyang'anya.
Hawaukabali ufukara na uchochole
wao. Ha, ha, ha, hahaha....
Wanastahiliiiiiiiiii kuuawa.
Hiyo ikafumbuka(midomo), akacheka, akacheka,
akacheka. Halafu ghafla
akasita. Akasema taratibu...
“La, hawastahili! Hawa wengine
wana kichaa kuliko yule mwizi”.
(uk. 110)

Mwandishi anatumia kicheko hapa na kuvuruta sauti kwa maana kinyume kuwasuta watu waliomuua kijana huyu. Ukatili wao wa kumuua siyo tofauti na ule wake wa kuiba.

4.1.4 Tashhisi

Kuhenga (1977) anasema kuwa neno tashhisi limezaliwa kutoka neno la kiarabu ‘shakhsia’ ambalo chimbuko lake lina maana ya ‘nafsi’. Tashhisi basi ina maana ya kunafsisha au kufanya kitu kuwa na maumbile au mahasa kama vile nafsi ya mtu.

Msokile (1993) anasema kuwa tashihisi ni tamathali ambayo vitu hupewa sifa zote au baadhi ya sifa za binadamu na kuonekana kutenda kama binadamu. Mtaalamu huyu na Kuhenga (1977) wanaielezea tamathali hii katika mazingira matatu. Kwanza ni mahasa na maono ya ndani ya binadamu kama vile dhamiri, choyo, mguu, chuki, nywele, njaa, furaha, kifo, mapenzi na fadhila au kasoro zingine za binadamu au sifa zinginezo za utu hunafsishwa na kupewa sifa za utu ili zielewekwe zaidi. Mazingira ya pili ni ya vitu visivyo na uhai kuwa na tabia za mtu. Vitu hivi ni kama moto, nyimbo, udongo, nchi, jua, milima, ukuta, gari, nyumba na kadhalika. Vitu hivi huvishwa taswira ya utu na kupewa maumbile ya wanyama au binadamu. Mazingira ya tatu ni tashhisi ya vitu vyenye uhai kama miti, wadudu, ndege na wanyama kupewa hulka ya wanadamu. Mwandishi ametumia tashhisi za aina zote tatu katika sehemu nyingi za *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, mhusika Mfuko Mtupu ana njaa na kiu ya maji hivi kwamba hangeweza kuhimili gilasi. Mwandishi anasema:

Aliipandisha nusu njia, gilasi.
ikatekemeka na matone ya
maji yakamwaika. Alipigana
nayo kuifikisha mdomoni na

hata ilipofika niliyasikia maji
mafunda kwa mafunda yanapiga
kasi kwenye koromeo lake,
yakatoa sauti kama vile
mio lake limeanza kuziba.
Na ghafla gilasi ikaponyoka na
kuanguka chini kwa mpasuko
na kurusha vigae huku na huko.
(uk. 3-4)

Mfuko Mtupu ‘kupigana na gilasi’ ni hali ya kuishikilia kwa nguvu na kujikakamua kuisogeza mdomoni. Maji ‘yakipiga kasi’ kwa mio yake ni hali ya maji kupewa sifa kwa kuteremka kooni mwake kwa haraka. Gilasi inapoanguka chini, vigae vyake vinatapakaa sakafuni kwa maana ya gilasi ‘kurusha’ vigae. Tashhisi hizi zinatupa dhuluma ya jamii kwa Mfuko Mtupu ya kukatalia pesa zake kama anavyodai.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, tunasoma:

Daudi aliupiga teke
mlango na mlango
uliokuwa haujafungwa
ulimtupa kwa urahisi
ukumbini mwake.
(uk. 26)

Mlango umepewa sifa ya binadamu ya ‘kumtupa’ Daudi ndani ya nyumba yake kwa maana ya, unafunguka bila shida unapogigwa teke. Mbinu hii inanasa nadhari ya msomaji pamoja na kuonya uozo wa Daudi wa kunywa pombe kupita kiasi.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia, mwandishi anaelezea hivi siku inayogonjewa kwa hamu ya kufika kwa Saada:

Uso wa mbingu ulianza
kukunjuka kukaribisha huru
ya jua.
(uk. 29)

Mbingu haina sura wala umbo. Mbingu inapopewa sura ya mtu ni tashhisi. Pia imepewa sifa za mtu za kukaribisha nuru ya jua, yaani kupambazuka. Maelezo haya yananata katika akili za msomaji na kumtia taharuki ya kutaka kujua siku hii ingekuwa vipi.

Pengine katika hadithi hii, huzuni ya wazazi wa Saada kabla ya kwenda Ulaya inaelezwa hivi:

Anayekwenda akirudi salama,
atakakuja kuauni nafsi yake,
wazee wake na jamii yake.
Ingawa upweke na ukiwa
uliowasimamia kati naye
ulilizia ndege mbaya.
(uk.30)

Upweke na ukiwa umepewa sifa ya kuwasimamia wazazi hawa, kwa maana ya kuwatawala. Dhana hizi ni dhahania na hazina miguu ya kusimama. Mbinu hii inaonyesha mapenzi makuu ya wazazi wa Saada kwake.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Sheikh Majid anapanga akutane na Maryam saa tatu usiku katika Forodha ya Mchanga. Kassim (Maryam) anapofika wa kwanza na kumsubiri mwenzake, tunasoma:

Alivuta mkono wa koti
lake na kutazama saa yake.
Saa nne juu ya alama usiku.
Saa ya Beit-el-ajaib na ile
yake mkononi hazikusema
uwongo.
(uk. 58)

Aina mbili hizi za saa zimepewa sifa ya kuzungumza kama mtu kwa maana ya kuonyesha wakati. Zinasisitiza kuwa maovu mengi duniani aghalabu hutendwa usiku.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, Naima anajipamba na kupambika. Mumewe Fumu akawa anamwangalia kwa upembe. Tunasoma:

Fumu ilimbidi kupiga kijicho
upembe kujaribu kulishibisha
jicho lake sirisiri uzuri wa
mkewe usiochujuka.
(uk. 130)

Jicho halina tumbo linalohitaji chakula. Mwandishi amelipa sifa ya ‘kula’ kwa maana ya macho ya mtu kukiangalia kitu au mtu kwa hamu kwa sababu yamependezwa na yanachoangalia. Tashhisi hii inamulika nafasi ya mwanamke katika jamii. Mojawapo ni kuchukuliwa kama pambo la kurembesha nyumbani au madhari fulani. Fumu anavutiwa sana na urembo wa mke wake Naima.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, Matwana akiwa mahakamani anasema hadharani bila woga kuwa jaji anayeisimamia kesi yake ndiye aliyemuua Uledi. Watu wanaposikia haya, wanashangaa.

Tunasoma:

Mshangao ukamea
mahkama nzima.
(uk. 144)

Mshangao ni dhana dhahania isiyoweza ‘kumea kama’ mbegu. Tashhisi hii ina maana ya watu walishangaa waliposikia kauli ya Matwana na mshangao ukaanza kuongezeka. Mbinu hii inaonyesha dhuluma inayotendewa wanyonge kama Matwana na wenye madaraka kama hakimu. Hakimu ndiye anafaa afungwe jela, si Matwana.

4.1.5 Tanakuzi

Kuhenga (1977) anasema kuwa fasili ya neno tunakuzi ni neno la kiarabu ‘nakuz’ ambalo lina maana ya ‘kuvunja’. Anafafanua tanakuzi kama mtindo wa uneni wa fasaha ambao kwao maono au mawazo mbalimbali yenye mgongano na uhitilafiano, huunganishwa pamoja katika sentensi au kifungu cha maneno ili kufanya mvutano mkubwa zaidi wa mawazo. Kwa mujibu wa Wamitila (2008: 508), kwelikinzani ni aina ya tanakuzi ambapo kauli au maneno yanayotumiwa huweza kuonyesha kupigana fulani katika kiwango cha kijuujuu ingawa katika kiwango cha ndani yana maana wazi. Katika kazi hii, hatujatofautisha dhana hizi mbili; tanakuzi na kwelikinzani kwa maana tumechukulia kuwa zina malengo sawa.

Kwa hivyo tanakuzi ni tamathali ya usemi inayoonyesha kinyume kwa kuweka sambamba maneno, kauli au sentensi ambazo zinakinzana ili kupata jawabu la maana linalotatiza au kupata msimamo maalum wenye mashiko kuhusu jambo fulani.

Mwandishi, Said A. Mohamed anatumia tanakuzi katika hadithi zake kwa mvuto mkubwa wa kunatisha hisia.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, ujaji wa Mfuko Mtupu pale mkahawani alipokuwa msimulizi unamwathiri sana mpaka pumzi zinampanda. Anaathiriwa na mwili, wasifu na hali yake Mfuko Mtupu mpaka hisia zake zinajipata katika njia panda, hazijui zichukue njia gani.

Tunasoma:

Picha nzima ilichusha
kwa hakika, ilisikitisha na
kushawishi wakati mmoja.
(uk. 1)

‘Kuchusha’ na ‘kushawishi’ ni tanakuzi kwa maana kuwa msimulizi anachukizwa na wakati huo huo anavutiwa na mchukuo wa Mfuko Mtupu. Mwishowe anachukua msimamo wa kumsaidia kwa kumuagizia sahani ya pilau.

Penginepo katika hadithi hii, msimulizi anakuza tanakuzi anapoendelea kumchunguza Mfuko Mtupu na kutanabahi kuwa anahitaji msaada wake. Tunasoma:

Nilitaka kumfunulia falsafa
ya kukosa na kupata.
Nilitaka kumwuliza kama
anajua nani anatoa na
nani anaenyima.
(uk. 3)

Mifano hii ya tanakuzi inafafanua hali ya umaskini na utajiri. Duniani, kuna watu walio na mali mengi na wengine ambao hata kupata maji ya kunywa ni shida kama Mfuko Mtupu. Mwandishi anaibua hisi zetu tujiulize ni nani wa kulaumiwa?

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana,’ maisha ya Mtama yalijaa dhiki za kupigwa na mumewe kila wakati. Mume huyu pia hawakimu kwa hivyo inabidi Mtama ajishughulisha kuwatafutia binti zao wawili chakula. Tunaambiwa:

Ndoa ilikuwa kwenda
na njia, jua na mvua
ukawa mchana wake
uliomshughulisha daima,
asijue arusini wala
matangani.
(uk. 24)

Tanakuzi za aina mbili zilizopigiwa mstari ni za kuonyesha hali tofauti za maisha; kukiwa na jua na mvua ni wakati wa furaha na huzuni. Tanakuzi hizi zinaelekeza kwenye maudhui ya masaibu ya mwanamke katika maisha hivi kwamba hatambui majira alimo.

Katika hadithi hii bado, masaibu ya Mtama yanapozidi, anafikiria kujiondoa uhai. Tunaelezwa na mwandishi kwamba:

Ilimjia rai ya nafuu ya
mwanzo aliyoitaka ya
kunywa asali ya mauti
na kumwacha Daudi katika
majuto.
(uk.25)

‘Asali ya mauti’ ni tanakuzi kwa sababu hakuna utamu katika kifo. Kwa Mtama, mauti yangukuwa matamu kwa sababu yangemuepusha na vipigo na matusi ya mumewe. Hili linaonyesha mtu huweza kukata tamaa ya kuendelea kuishi masaibu yanapomzonga.

Katika hadithi ya ‘Mhanga na Mwanamaua’, wanakijiji wa Pemba wanajitumbuiza kwa mchezo wa kutazama ng’ombe wakiwakimbiza watu katika uwanja wa Wingwi.

Tunasoma:

Machumi ya karafuu huja
na furaha na misiba yake
(uk. 82)

Wanapemba wanafurahia neema ya kuchuma karafuu na pia kuomboleza vifo vya wale wanaoshindwa kuwaepuka ng’ombe na hivyo kuuawa. Dadi anakuwa mmoja wa wanaouawa na ng’ombe Kipelele. ‘Furaha’ na ‘misiba’ yao inaonyesha uhalisia wa maisha ya kufurahi na kuhuzunika.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda anahamia mjini baada ya kupoteza mali yake na mkewe akafa. Siku hii ya kwanza mjini amevalia mararu na watoto wanapomwona wanamfukuza na kumwita mwendawazimu huku wakicheka na kufurahi.

Tunasoma kuwa kwa watoto furaha yao ilikuwa ‘furaha katika mauti yake’(uk. 116). Furaha ya watoto ya kumbandika Mwenda uwendawazimu katika msiba wake mkuu ni kama mauti kwake.

Tanakuzi hii inaonyesha ukosefu wa huruma miongoni mwa jamii hasa kwa wale wanaoumia.

Wakati mwingine hali hii hutokana na kutojua ukweli wa mambo.

4.1.6 Majazi

Wamitila (2002: 25) anasema kuwa majazi ni ufundi wa waandishi wa kazi za kifasihi kuyatumia majina ya wahusika ambayo huakisi mandhari zao, wasifu wao, tabia zao, itikadi zao, vionjo vyao, n.k. Majazi pia huhusisha majina ya mahali. Majazi humsaidia msomaji kufahamu sifa na

tabia ya wahusika, kubainisha msimamo wa mwandishi kuhusu wahusika wake mbali na kuchangia kukuza maudhui yake.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’, mhusika Mfuko Mtupu anapewa jina la kimajazi. Ingawa anasema kwamba alikuwa mwalimu kwa miaka mingi, kwa sasa hana kitu. Hawezi hata akajinunulia chakula wala kinywaji katika mkahawa. Ana ukiwa wa mkewe kwani mwenye mkahawa amemchukua. Hajui mwanawe aliko, yaani hana kitu wala watu wake karibu naye. Mwandishi anatumia majazi haya kukuza maudhui ya umaskini.

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’, jina Mwanamaua ni la kimajazi. Mwandishi anasema kuwa kule kisiwani Pemba, binti akipewa jina hilo anapozaliwa, huwa amepewa jina la kinga, maana hukabidhiwa pepo mashuhuri amlinde na husuda za ulimwengu. Maua ni mmea unaopendeza kwa maua yake na unaovutia wengi wakiwemo wadudu na binadamu. Mwanamaua anamwambia Dadi mchumba wake kuwa aliwakataa vijana wote wa kijiji chao akamchagua yeye. Wanaume wanavutiwa naye kama vile ua huvutia kwa urembo wake. Jina hili linarejelea hekaheka za uchumba ambapo msichana mmoja hupiganiwa na wengi.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, jina Mwenda ni la kimajazi. Mwenda linatokana na kitenzi ‘enda’ cha mtu anayetembeatembea huku na huko bila kutulia. Mwenda anapofilisika na mkewe akafa, anahamia mjini, maskini hoehae. Alikuwa anazurura mjini bila makao maalum huku akicheka. Hakuwa na kazi yoyote pia. Tunasoma kuwa Mwenda ambaye si mwendawazimu, alikuwa ‘mwenda-na-njia’ (uk. 107). Tena mwandishi anasema, ‘Baadaye aliendelea na safari yake’. Mwenda hana pahala maalum pa kwenda, ila anatambatamba kutafuta kitu cha kulipatia chochote tumbo lake (uk. 113).

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, kuna mhusika Naima Mambo ambaye anelezewa hivi:

Ukisikia Naima Mambo ndiye
huyu. Ana mambo kushinda!
Anaweza kukigonganisha kijiti
kwa chuma navyo vikawaka
moto na kugeuka jivu. Kwa
umbo mkamilifu. Kwa mizungu
kungwi kwa makungwi.
(uk.130)

Mambo ni shughuli nyingi anazofanya mtu. Naima Mambo ni majazi yanayomwafiki mhusika huyu kwa sababu anapanga njia thabiti ya kumfumania mumewe Fumu aliyekuwa mzinzi na hatimaye anafaulu. Anajifanya kuwa mmoja wa makahaba katika danguro alimoenda mumewe na kweli mumewe anamfumania huko. Hamtolei ukali mumewe bali anamshika mkono na kumwambia warejee nyumbani.

Hadithi hii pia ina mhusika mwingine anayeitwa Mama Kitimbi. Kitimbi ni kitendo cha hila au cha kudhalilisha kinachotendwa dhidi ya mtu fulani kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya 21* (2011). Mama Kitimbi ni mmiliki wa ‘duka la laana’ (uk. 134). Anafanya biashara ya kuwauza wasichana na wanawake kwa wanaume wazinzi kama Fumu ili apate mali. Anawaita wasichana wake malaika na kumfahamisha Fumu alikuwa amepokea kitoto kipya ambacho angelipia milioni kustarehe nacho. Kazi ya Mama Kitimbi ni ya kudhalilisha na kutukanisha jinsia ya kike. Jina la Mama Kitimbi linaonyesha uozo wa ukahaba miongoni mwa wanajamii.

4.1.7 Tasifida

Kuhenga (1977) anasema kuwa tasifida ni msembo wa adabu ambao kwao, mambo yasiyopendeza hutamkwa na hasa hadharani, kwa lugha ya siri bila kuchukiza au kuchafua moyo ili kuficha kinyaa au hali mbaya waonayo watu moyoni. Jamii nyingi zina makataa ya kutumia lugha ya uwazi hasa kuhusiana na uchafu wa matusi au karaha ya aina fulani. Jamii hutumia kauli za mzunguko au mafumbo kutaja dhana na matendo yanayohitaji siri.

Tasifida imetumika katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’. Sheikh Majid anamuasa Kassim kwa kumwambia:

hakuna maasi makubwa
duniani hama ulevi na
kuchuma matunda
(uk.55)

‘Kuchuma matunda’ ni lugha ya adabu inayomaanisha ‘kulala na wanawake’. Usemi huu unapunguza ukali wa ushauri huu ili Kassim asiaibike sana.

Tasifida nyingine inapatikana katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’. Mwanamaua na Dadi wanakutana usiku mmoja nje. Wana siku saba kabla ya kuasi ukapera na hamu zao mmoja kwa mwingine ziko juu. Tunasoma:

Dadi alisogea, akanyoosha mikono
yake na Mwanamaua akaishika
hodari! Walisimama hivyo kwa
muda. Hatimaye wakajitupa
chini kwenye majani na
muda wote wakawa bado

wameshikana katika ile
faragha. Wote walivutwa na
ukweli uliowajaa mioyoni
mwao. Ukweli waliungojea
kwa hamu, kwamba bado siku
saba tu, dhiki ya kukutana
msituni itaondoka.

(uk. 78)

‘Kujitupa chini kwenye majani ili kumaliza dhiki ya kukutana msituni’ ni tasifida ya kumaanisha kuwa walifanya mapenzi, wakijificha wasionekane. Kitendo chao kinaonyesha tamaa na uchu mkuu unaowajia vijana wawili wanaodhamiria kufunga ndoa.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Siraba anakumbwa na makubwa baada ya kurejea nyumbani kwao. Anatoka Köln Ujerumani baada ya kuishi huko kwa miaka ishirini.

Tunasoma:

Baada ya kufika nyumbani
bila ya shaka amekuta
aliyoyakuta na ameyasikia
aliyoyasikia

(uk. 119)

‘Amekuta aliyokuta’ ni tasifida yenye maana alikuta tayari mamake mzazi, Mama Mkaja amekufa. Maneno ‘amesikia aliyoyasikia’ ni tasifida ya kumaanisha anasikia kuhusu kufilisika kwa babake mzazi, bwana Mwenda na kuhamia kwake mjini anakopatwa na kichaa. Tasifida hizi zinapunguza makali ya kumwarifu Siraba hatima ya wazazi wake na kumpunguzia kuchafuka kwa moyo wake.

Tasifida nyingine zinapatikana katika hadithi ya ‘Njia Fupi’. Fumu anawachwa na mkewe Naima nyumbani kwao bila kumwambia anaokokwenda. Naima alikuwa amejirembesha kwelikweli mpaka akamtia mumewe tamaa. Tunasoma:

Alikuwa kama paka shume
lazima atoke akawinde.
Na mahala mwafaka ni
kwa mama Kitimbi.
(uk. 133)

Tashbihi ya paka shume aliye na hamu ya paka jike inatia mkazo tamaa ya Fumu kumtaka mwanamke. ‘Awinda’ ni tasifida iliyo na maana ya ‘akatafute malaya’ kwa danguro ya Mama Kitimbi. Tasifida hii inapunguza aibu ya msomaji kujua vitendo vyake ilhali yeye ni mtu aliyepoa.

Kwingineko tunasoma Fumu anaenda kwa Mama Kitimbi ili ‘kujaribu kuzimua joto lake la roho. Ukitaka kuondoa maudhui zipishe tulizo ziingie moyoni mwako! Furaha iliyoje kupata liwazo la maana baada ya vile vitimbi vya Naima leo’. (uk. 135)

Maneno ya ‘tulizo’ na ‘liwazo’ ni maneno ya tasifida kwa maana ya kufanya mapenzi. Tasifida hii inaondoa aibu inayotokea tunapobaini lengo la Fumu la kwenda kwa danguro ya Mama Kitimbi. Alikuwa mzinzi.

Baadaye, Fumu anapofumaniwa na mkewe huko danguroni tunasoma:

Hakuelewa Naima alijuaje
kwamba ni mtembelea na
mshiriki wa matendo ya
nyumba hiyo.
(uk. 135)

4.1.8 Maswali ya Balagha

Kuhenga (1977) anasema kuwa tamathali ya balagha ni msembo wa tashtiti ambao kwao mwandishi hutoa hoja za kuisimua au kuuliza maswali ya kuchoma chuki ambayo huchochea furaha, huzuni, chuki na mzinduko wowote wa utendaji, ili kushawishi mtu atende jambo fulani zuri au baya. Maswali ya balagha hayahitaji majibu. Humsaidia mhusika wa hadithi na msomaji kufikiria kwa kina na kuchukua hatua fulani panapobidi.

Hadithi ya 'Pigo Kupokezana', inianza kwa maswali ya kitashtiti kwa Mtama. Tunasoma:

Lipi linalompa Mtama ameze
mrututu hali anajua mchungu?
Lipi linalomfanya asogonee
dhiki na kushindiliwa pumzi
moto? Lipi linalompelekea
asalimu amri wakati mdhi-
biti wa umri ni
yeye mwenyewe? Lipi
linalompa ang'ang'anie
wakati uamuzi wa kukubali
na kukataa umo
mikononi mwake?
(uk.22)

Maswali haya yanamchochea Mtama achukue hatua ya kukomesha dhuluma anayopokea kutoka kwa mumewe. Mwishowe anakunywa dawa ya kupoteza fahamu kwa muda na kuzindua mumewe kuona udhalimu wake, akabadilika. Maswali haya yanapinga vikali uovu wa Daudi kwa mkewe wa kumpinga na kumtusi.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda anajiuliza maswali mengi baada ya kushuhudia kijana mmoja aliyeiba akipigwa hadi kufa. Anajiuliza:

Yeye kweli aliiba. Kweli
wamemkamata. Lakini kwa
nini walimhujumu? Kwa nini
walimwua? Kwa nini wamechukua
sheria mikononi mwao?
(uk. 110-111)

Maswali haya ya Mwenda hayahitaji majibu kwa maana majibu yanajulikana. Mwandishi ameyatumia ili kushambulia uovu wa raia kumuua mhalifu badala ya kuwaachia walinda usalama. Yanaonyesha chuki yake kwa watu hawa kwa sababu hata hao ni wabaya.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’ Matwana anajiuliza maswali mengi usiku wa kuamkia kupelekwa kwake mahakamani kujibu mashtaka ya kumuua Uledi. Ingawa anajua ukweli wa mauaji haya alikuwa amekataa kuusema. Tunasoma:

Siku ya hukumu imewadia
Je, atanyamaza kama alivyonyamaza
mwezi mzima, au atasema kweli
awaonjeshe chungu wapanga
uwongo? Je, akisema ukweli,
itanusuru roho yake hii inayotaka
kudhulumiwa? Afanye nini?
Ajinusuru vipi?
(uk.138)

Maswali haya ya kitashtiti yanaonyesha mtafaruku wa ndani kwa ndani wa Matwana kuhusu kesi yake. Hatimaye yanamsaidia kufanya uamuzi wa kusema ukweli kuhusu muuaji wa Uledi; anachukua hatua ya kuongea hata kama angefungwa kwa kosa ambalo halikuwa lake.

4.1.9 Chuku

Mohamed (1995) anasema kuwa chuku (anayoiita kitia –chumvi) ni mbinu ambayo hukuza jambo liwe kubwa kuliko lilivyo kawaida na kwa mujibu wa Kuhenga (1997) jambo dogo hudunishwa kupita kiasi. Mbinu hii ya lugha aghalabu hutumiwa kwa dhamira ya kuisitiza au kukuza kitu na pia kupunguza sifa za kitu au mtu kwa madhumuni ya kudunisha.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ msimulizi anaeleza maumbile ya Mfuko Mtupu kwa njia wazi.

Alikuwa amevaa mararu na manywele yake ni timtim. Anaongezea kusema:

Kijuso chake kilichokondeana
kilikuwa kimefichwa na chaka
la masharubu.
(uk.2)

‘Chaka’ ni eneo kubwa la miti mingi. Mwandishi anatilia chumvi masharubu mengi ya Mfuko Mtupu kwa kusema ni kama chaka. Chuku hii inatilia mkazo umbo la kuogofya la Mfuko Mtupu.

Penginepo katika hadithi hii baada ya Mfuko Mtupu kukataa kununuliwa chakula na msimulizi, anachomoka ghafla kwenye mkahawa na hapo nje anapigwa dafrau na gari na anakufa. Mpita njia mmoja anaeleza hivi:

Kafa kipovu kinamtoka kwa
njaa ya mwaka mzima.
(uk.7)

Maneno ya ‘njaa ya mwaka mzima’ ni chuku na ni kutilia mkazo dhiki za Mfuko Mtupu ambaye hawezi hata kujilisha kwani mtu hawezi kukaa mwaka mzima bila kula.

Hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’ inaendeleza chuku kwa kuonyesha idadi kubwa ya wanaume inayomtaka Mtama awe mkewe. Tunaeleza:

Au makundi kwa makundi
yao wanapomzonga alipokuwa
akitembea njiani. Alipita akijitupa
na kujitikisa akikanyaga ardhi yake ya
ujana. Hakuna moyo wa mwanamme usio-
tuturishwa na umbo hili.
(uk. 23).

Ni chuku kusema makundi ya wanaume yanamfuata Mtama njiani yakimtaka. Kutumia neno ‘hakuna’ ni chuku kwa sababu si wanaume wote wanaopendezwa na umbo la Mtama. Tamaa ya wanaume kwa Mtama imepanuliwa sana ili kusisitiza uzuri wake na kuonyesha kinyume cha mambo wakati Mtama anamchagua Daudi maskini kuwa mume wake.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, mavazi ya Saada ya aibu kwa wanakijiji wake yanapigwa chuku ili kuonyesha athari za kupapia tabia za kigeni. Mwandishi anasema kuwa suruali ya Saada ‘ilikuwa imembana na kubainisha viungo vyake vya siri waziwazi’ (uk. 33).

Hii ni chuku kwa sababu huwezi kuona sehemu za siri za mtu waziwazi iwapo amevaa suruali.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’ kuna chuku pale ambapo Mama Kitimbi anamwambia Fumu kuwa siku hiyo angelipa milioni nzima kwa kujistarehesha na Naima. Milioni nzima ni chuku inayozidisha sana pesa wanazotoa wanaume kwa kwenda kwa danguro la Mama Kitimbi. Maneno haya yanatilia mkazo tamaa yake ya pesa.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, mwandishi anatumfahamisha kuwa Matwana hakuwa amelala kwa mwezi mzima tangu afungwe jela (uk.137). Hii ni chuku kwa maana binadamu wa kawaida asipolala mwezi mzima huenda akaugua. Chuku hii inatilia mkazo sumbuko la Matwana la kutiwa jela kwa makosa ya mtu mwingine.

4.2 Mbinu Nyingine za Lugha

Mbali na tamathali za usemi ambazo tayari tumeshughulikia, zipo mbinu nyingine muhimu katika uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Mbinu hizo ni pamoja na;

4.2.1 Takriri

Msokile (1992:60) anasema kuwa takriri ni marudio ya sauti, silabi, neno, sentensi wazo au ridhimu. Lengo kuu la takriri ni kutia mkazo au msisitizo kuhusu jambo linalozungumziwa.

Katika hadithi ya ‘Mfuko Mtupu’ kuna takriri ya sauti ‘ki’ kuisisitiza wembamba wa uso wa Mfuko Mtupu ambao ni ishara ya njaa. Tunasoma:

Kijuso chake kilichokondeana
kilikuwa kimefichwa
(uk.2).

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’ kuna takriri ya neno ‘hasara’. Bwana Haji anamfariji Miraji asimjali bintiye anayewadharau na hata kurudi mjini siku ile alifika. Anasisitiza kuwa majuto ni yake Saada bali si yao. Anakariri:

Baba, usijali...hasara ni
yake siyo yetu: hasara
ya kukataa mikono
iliyomleta duniani na

kumlea na wenzi walio-
changamka na kucheza
naye – hasara kubwa kwa
mwenye kujua
(uk. 35).

Takriri nyingine imo katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’. Takriri hii ni ya silabi ‘aka’ inayoeleza vitendo vya Mwanamaua anapotoka kwao kwenda kukutana na Dadi. Anaenda huku akiondoa vikwazo vyote njiani ili afike mahala pao pa mkutano. Takriri hii inatilia mkazo nia ya Mwanamaua ya kumwona mpenzi wake. Tunasoma:

alikuwenda kwa dhamira
huku akijikwaa. Alikata
gugu lilimsonga miunduni
mwake. Akasepetuka
karibu asinukie.
Akajiokota. Akasita.
Kisha akatimka kwa
nia na hamu kubwa
zaidi. Akapita akivivaa
vimulimuli.
(uk. 77)

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda anavunjika moyo kwa masaibu yanayomfika. Anauza ng’ombe na shamba lake, mkewe anakufa na mwanawe anakataa kurejea nyumbani; hata salamu hatumi. Uchungu wa Mwenda unaelezwa kwa takriri ya maneno ya kukata tamaa ili kuusisitiza. Tunasoma:

Ghaffla alipata msiba wa
kufiwa na mkewe Mama
Mkaja; na hapo ndipo alipo-
kata tamaa na kujua sasa
dunia yote imempa mgongo.
Alikata tamaa kwa maana
ya kukata tamaa.
(uk 116)

Huku kukosa matumaini kunamwelekeza kuuza nyumba yake na vitu vyote vilivyobakia akajikuta fukara.

4.2.2 Usambamba wa Visawe

Usambamba ni urudiaji neno, maneno au sentensi. Visawe ni istilahi inayoashiria uhusiano wa kimaana baina ya maneno.

Mohamed (1995: 131) anasema kuwa wanaisimu wanaeleza vyema kanuni muhimu kwamba, maneno mawili hayawezi kusimamia kwa ukamilifu maana moja kwenye mazingira yaleyale. Mwandishi mahiri wa nathari ya Kiswahili anatarajiwa awe na hazina ya viko vya maana vyenye visawe vyake vinavyojitokeza katika kazi yake.

Usambamba wa visawe hutumiwa ili kutilia mkazo wazo, dhana au maana fulani ya ujumla. Lugha ya Mohamed imethibitisha ukwasi wake wa visawe kwa mifano hii.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, tunasoma:

Mtama alikuwa Mtama
kweli! Wacha ndege waru-
keruke na kutua nyumbani

kwao kwa mbinja na miunzi
na ushaufu na matamano
(uk 23).

‘Mbinja’ ni ‘miunzi’, ni muziki unaotoka midomoni mwa watu. ‘Ushaufu’ ni hali ya matamano ya kibinadamu ya kutaka kufanya mapenzi. Seti hizi za maneno ni visawe vinavyotilia mkazo mbinu wanazotumia wanaume ili wamnase Mtama.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, wazazi wa Saada wanamlea hadi pale wanapolazimika kuumkabidhi ulimwengu jukumu la kumlea mwana wao katika masomo huko Ulaya. Tunasoma:

ndipo miaka mitano iliyopita
wazee hao wawili walifikwa
na msiba wa kumtoa mtoto
wao mmoja wa kike na
kuusabilia ulimwengu wa kigeni
wasiojua heri yake wala shari
yake. Huo waliupa dhamana ya
kumtunza na kumduhushi
binti yao.
(uk. 29)

‘Kumduhishi’ ina maana ya kumtunza, kumwanguka na kumhudumia mtu kwa karibu. Hivi ni visawe kutilia mkazo kuwa ulezi wa mtoto si wa wazazi tu mbali jamii huchangia.

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, Mwenda alipouza mali yake yote, anabaki maskini bila kitu. Tunaeleza:

Taratibu Mwenda aliporomokea
ufukarani, akauza nyumba yake
na vyote vilivyombakia. Yote ni
kwa haja na uhitaji. Alipotahamaki
alikwenda kapa na rafiki zake
wanya sasa walikuwa uchochole
na ulitima. Akabaki mtupu.
(uk. 117)

‘Ufukara’ ni maskini au uchochole wa kupindukia. ‘Kwenda kapa na ‘ulitima’ ni hali ya kuishiwa na pesa. Visawe hivi vinatilia mkazo umaskini wa Mwenda.

4.2.3 Tanakali za Sauti

Tanakali za sauti ni neno linalotokana na mlio wa kitu ambacho linakiwakilisha, kwa mujibu wa Massamba (2004:86). Neno hili linaloiga sauti ya kitu hutoa picha ya kitu kinachowakilishwa na sauti hiyo na inayotolewa.

Tanakali ya sauti inatumiwa kueleza hali aliyokuwa Daudi anaporudi nyumbani kwake na kumpata mkewe ‘amekufa’ katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana.’ Tunasoma:

Siku hii kama kawaida
ya Daudi alirudi nyumbani
kwake saa nane za usiku –
chopi! Anayumbayumba
(uk.25)

Daudi kulewa ‘chopi’ si kielelezo kizuri cha uzazi bora.

Aidha katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, ukware wa Sheikh Majid unafafanuliwa zaidi na tanakali ya sauti hii:

Lo, Majid gani nazo zisizoenda
dobi zikatakata. Babu we, hamna
shehe pale! Lo, Bwana yule mjalana.

Kisipite kibuibui. Asisikie ndara
masikio twii yamemsimama.
(uk.57)

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua,’ tanakali ya sauti inatumiwa kuonyesha jinsi ng’ombe Kipelele alimteka Dadi na kumrusha juu hewani na anapoanguka, anavunjika shingo. Tunasoma:

Dadi hakuwahi kukwepa
na Kipelele alimteka na
kumrusha juu hewani.
Pu! Alianguka Dadi
akafikia kichwa na
hakuonekana kuinuka,
(uk.85)

Katika hadithi ya ‘Kicheko cha Mwendawazimu-Akili’, kuna kicheko cha stihizai kwa raia wanaompiga kijana mwizi. Kicheko chake kinashutumu mauaji haya. Tunasoma:

Kwa nini hawawezi kukinai?
Wanaiba... kwe, kwe, kwe, kwe.
Alicheka tena.
(uk.110)

4.2.4 Kuchanganya Ndimi

Haya ni matumizi ya lugha nyingine katika matini kando na lugha ya uandishi. Hudhihirika pale ambapo neno la lugha nyingine hujitokeza katika kazi ya fasihi kwa maendelezo na matamshi ya lugha asilia. Kwa mfano, matumizi ya maneno ya Kiingereza au Kiarabu au hata lugha nyingine katika kitabu cha Kiswahili ni kuchanganya ndimi.

Katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, Saada anachanganya ndimi. Baada ya kwenda Ulaya kusomea uwakili kwa miaka mitano, anarejea kwao akiwa amebadilisha mavazi, maumbile na hata lugha yake. Mwandishi anaeleza kuwa alizungumza kwa kiimbo cha kizungu.

Anasema:

'Good gracious', alibwata Saada,
kundi lote lile limekuja kufanyaje?
(uk.33)

Mamake Bi. Mhando ametayarisha vyakula vya aina mbalimbali kwa bintiye Saada lakini anavikataa kwa dharau. Anasema:

My ... its not me .. nani
atakula dirt? Baadaye
Saada alikwenda garini
na kutoa vyakula vya
kibati katika buti, akakaa
juu ya domo akala.
(uk.33)

Huku kuchanganya ndimi kunadokeza maudhui ya elimu ya nchi za nje na pia ukengeushi wa kupuuza vya asilia na kutaka vya kigeni.

Aidha, mwandishi amechanganya Kiswahili na Kiarabu katika hadithi ya 'Nyuma ya Pazia'. Tunasoma:

Tubia kwa Mungu wako...
sema staghafiru Ilah, dunia
mbaya mwanangu.
(uk.56)

'Staghafiru Ilah' ni msemu wa kidini wa kutubia kwa Mwenyezi Mungu kwa makosa uliyofanya. Shehe Majid anamsihi Kassim atubie makosa yake ya ulevi na kuchuma matunda.

4.2.5 Jazanda

Baadhi ya wataalam wanaeleza taswira kama picha inayojengeka akilini kutokana na kusikia au kusoma matini fulani. Jazanda nayo ni kile kinachoashiriwa na picha hiyo. Kazi hii inachukulia kuwa jazanda ni taswira au picha inayotokana na maelezo yanayotumia maneno haya kutoa maana wazi au fiche.

Said A. Mohamed anatumia taswira kadhaa katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, tunaweza kuona katika akili zetu athari ya ‘kifo’ cha Mtama kwa Daudi mumewe. Alilia hadi ya kulia. Tunaelezwa:

Dunia ilikuwa nyembamba
mno kwa Daudi. Aliona inambana
na pumzi hapati, kijasho kilimtoka,
mwili ukamtetemeka na moyo
ukampiga beni. Daudi alijiangusha
juu ya kiwiliwili cha maiti
akakikumbatia. Alilia. Alilia kwa kekefu.
Alilia mpaka machozi yakawa sehemu
ya kiwiliwili chake. Lakini hatimaye,
katika kakasi za kilio alihisi mkono
umewekwa begani pake.
(uk.27)

Taswira hii inaonyesha majuto ya Daudi kwa mateso anayomtendea mkewe Mtama.

Aidha, katika hadithi ya ‘Tumba Iliyovia’, mwandishi anatupa picha/taswira ya Saada alipotamalaki kutoka Ulaya. Amebadilisha mavazi, uso, tabia na wanakijiji wanaona aibu kumwangukia. Wazazi wake wanaangukia chini kwa aibu hadi wanaomba ardhi ipasuke waingie. Taswira hii inatumia tashbihi, tashhisi na tabaini kuonyesha maudhui ya kuacha mila za mtu na athari zake. Tunasoma:

Saada alisimama,
sanamu, sanamu si sanamu,
mtu si mtu – mkavu kakauka,
uso umefinga na hasira
zisizomstahili zinamwenda
na upungufu unampwita
mdomoni. Miraji aliyekuwa
kasimama mbele ya watu

na kutaka awe wa mwanzo
kumlaki Saada, alipigwa na
bumbuwazi. Akamkagua Saada.
Nywele zake zimebadilika. Badala
ya visokotero sasa ni singa isiyo ya
maumbile. Uso wake mweusi sasa
ulikuwa mweupe kama shetani.
Nyusi zake nene za kifungo sasa
nyembamba kama uzi. Na
Shingoni dani la kete linaning' inia
hadi tumboni. Juu kavaa kishati
kilichofunguliwa vifungo na
kuacha madodo ya kifua chake
wazi. Hakuwa amevaa sidiria
kamwe!

(uk.32)

Kisa cha Saada kinafanana na cha mhusika Monika katika riwaya ya *'Mwisho wa Kosa'* ya Burhani (1987). Monika ameenda Ulaya kwa masomo zaidi. Anaporejea kwao, amebadilika kimavazi, kifikra na kitabia. Katika uwanja wa ndege, anateremka kwa mikogo akiwa amevaa shati, suruali na viatu vya visigino virefu. Amekata nywele zake na kuzitumua kwa mtindo wanaoupenda vijana. Anakataa kuwasabahi walioenda kumlaki ila jamaa wake tu. Anapofika kwao, anakataa kula chakula walichomwandalia akisingizia ni kichafu. Siku zinapoendelea kupita, Monika anaendelea 'kuwapuuza na kuwakunjia uso wote waliokuwa wenzake'.(uk.4). anapopata kazi, anakataa kuwasaidia wazazi wake maskini. Elimu yake Ulaya inamkengeusha si haba hadi kufikia kupuuza yote ya kwao huku akitukuza ya huko Ulaya.

Katika hadithi ya 'Kicheko cha Mwendawazimu-Akili', tunapata taswira ya Mwenda anapojiangalia kwa kioo cha gari moja maegeshoni. Muda wa miaka kumi na mitano akiishi mjini umembadilisha. Mwandishi anaandika;

Alijiona. Kwanza alirudisha uso
wake kwa woga. Akashangaa kwa
muda mfupi. Kwisha akajiangalia
tena. Aliutazama uso wake
uliomparama, akajaribu kuipuuza
ile mikunjo iliyokuwa ikipiga kasi
hapo. Macho yake madogo yalikuwa
yamezama kwenye matundu yake.
Kipaji kimetoka nje na kufanya komo.
Fupa la shavu na kidevu limechomoza
kiasi cha kuzuiwa na maki nyembamba
ya ngozi yake.
(uk.113)

Penginepo katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, tunapata taswira ya makahaba wanaojiriwa na Mama Kitimbi kuwafurahisha wanaume kama Fumu. Walikuwa wamesimama mstari mmoja. Wanaonyesha kutamaukwa kwa binadamu hadi kufikia kujiuza miili yao ili wajikimu.

Tunasoma:

Naam, wanawake wa sura
mbalimbali, wengi vijana,
wengine makamu. Kuna
baadhi walitia fora na
waliokubuhu. Jicho la
Fumu lilikwenda taratibu,
lakini halikufika mwisho!
(uk.135)

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, hakimumu anaamua kwamba Matwana ni muuaji na kuamuru anyongwe mpaka afe. Uamuzi huu unamuathiri Matwana, familia yake na wote waliokuwa. Mwandishi anasema:

Matwana machozi yalimmiminika!
Ukumbi mzima wa mahkama ulijaa
minong'ono na malalamiko na katika
vuguvugu hili sauti nyembamba ya
ukwenzi wa mwanamke ilipasua na
vilio vikafuatia – vilio vya mama na
watoto wake.
(uk. 145)

Tunaweza tukayaona machozi ya Matwana Kusi na kusikia kilio cha mkewe na watoto wao kwa sababu ya uamuzi wa dhuluma wa hakimu. Matwana siye muuaji.

4.2.6 Methali

Methali imetolewa fasili nyingi katika kuielezea. Mbatiah (2001:45) anasema kuwa methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha ukweli na busara. Kwake, methali zinabeba mila, falsafa, miiko na desturi za jamii. Msokile (1993:44) anaongezea maelezo haya kwa kusema kuwa methali hutumia mafumbo. Kazi yake ni kutoa hekima, kufurahisha, kutisha, kuonya na kadhalika.

Said A. Mohamed ametumia methali sampuli nyingi katika msururu wa hadithi zake fupi. Katika hadithi ya 'Pigo Kupokezana', mwandishi anasema, 'Paka akiondoka, panya hutawala ehh! (uk.26). Methali hii inatamkwa na Daudi. Anajilinganisha na paka na Mtama mkewe ndiye panya. Anasema haya anapomwita Mtama amfungulie mlango bila kupata jawabu. Kwake, ule ukimya ni ujeuri ndiposa anatumia methali hii kwa maana ya kiongozi (yeye) akiondoka, walio chini yake (Mtama) huchukua usukani. Methali hii ni kinyume cha mambo kwake kwa sababu Mtama hakuwa na sauti katika ndoa hii.

Katika hadithi ya 'Tumba Iliyovia', wazazi wa Saada wanalazimika kuuachia ulimwengu umlee binti yao anapopata fursa ya kwenda ng'ambo kusoma. Hawana uwezo wa kuzuia kwenda kwake Ulaya. Ndiposa mwandishi anasema, 'Lisilo budi huwa.'(uk.29).

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Kassim anamuwekea mtego Sheikh Majid ili athibitisha ukweli wa maneno ya Maryam. Mhusika Maryam amemwambia kuwa Sheikh alikuwa amemsumbua siku nyingi akimtaka kwa mapenzi. Kassim anamwandikia barua Sheikh Majid akajifanya yeye ni Maryam na kumtaka wakutane ufukweni katika Forodha ya Mchanga. Mwandishi anasema kuwa Sheikh Majid anaenda ufukweni akiwa na furaha na kusema, ‘Ama kweli subira huvuta heri.’(uk,59). Kwake, uvumilivu wake umezaa matunda. Methali hii ni onyo kwa wenye tamaa za ukware za kuvumilia kutendeka kwa jambo lile hata wakijua si haki.

Hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’ ina methali inayosema, ‘kwa mwoga huenda kicheko na kwa shujaa kilio.’ (uk.81). Dadi ni kijana mwenye huruma, mcheshi na mwenye bidii katika kazi za ukulima na ufugaji. Mwanamaua harithishwi na haya na anamdhihaki kwa kumwambia kuwa yeye ni mwoga maana hajawahi kupigana na wenzake akiwa mdogo wala kucheza uwanjani na fahali wakali. Mwanamaua anamtaka aende achezze. Dadi haoni haja ya kucheza na ng’ombe hatari kwa sababu huenda akapata msiba kwa ushujaa wake. Afadhali kuitwa mwoga na kuendelea kucheza. Methali hii inaonyesha busara ya Dadi ya kujiepusha na mchezo hatari wa kuchezea ng’ombe.

Katika hadithi ya ‘Njia Fupi’, mwandishi anasema, ‘Tabia ya mwanadamu ni ya uambangoma, kila mmoja huvutia kwake’. (uk.131). Mwandishi ametumia methali hii akimrejelea Fumu anayetaka kujitoa lawamani kwa kuwa na jicho la nje. Fumu anasema kuwa hawezi kujizuia na daima hujifikiria kwanza bila kujali hata kama angesaliti mapenzi ya mkewe Naima. Methali hii inatumiwa kuonya waliojawa na uchoyo wa ubinafsi wawe wanawafikiria wengine pia.

Katika hadithi hii hii, Mama Kitimbi anatumia methali mbili kurejelea umuhimu wa siku hii. Mama Kitimbi amepokea kisura kipyra katika danguro lake na anataka kumtia hamu Fumu ya kutazamia siku hii. Anasema ‘Leo ndio leo asemaye kesho mwongo! Leo ni leo, asiye mwana aeleke jiwe’(uk.134). Tena Mama Kitimbi anamjuzia Fumu kuwa, ‘Na kwa mwenye macho hambwi tazama; (uk.134). Methali hii inamtayarisha Fumu na kumjaza hamu kutolea joto lake pale ili kuimarisha maudhui ya mapenzi nje ya ndoa.

Katika hadithi ya ‘Hukumu’, baada ya Matwana kunyamaza kwa muda wa mwezi mmoja

mahakamani bila kujitetea, anaamua kuongea na kuifahamisha mahakama ukweli wa mambo na ‘Liwe Liwalo’(uk.144). Alikuwa anahofia usalama wake kwa kusema ukweli wa kifo cha Uledi. Hatimaye, anaamua atasema ukweli hata kukitokea nini. Methali hii inaonyesha busara ya kusimama thabiti na ukweli ujuao.

4.2.7 Barua

Barua ni maandishi yanayotumwa kwa mtu na yenye ujumbe fulani na ambayo hutumwa kwa njia ya mkono au kupitia kwa posta au njia ya elektroniki. Mwandishi ametumia barua katika diwani yake kama mbinu ya kupitisha ujumbe na kukuza maudhui kwa njia inayoongeza uelewekaji.

Katika hadithi ya ‘Pigo Kupokezana’, mwandishi ametumia barua mbili kupitisha ujumbe wake. Barua zote zinandikwa na Mtama kwa mumewe Daudi. Mtama anapochoshwa na vipigo na matusi ya mumewe ya kila siku, anamua kuchukua hatua ya kukomesha dhuluma hii. Ananunua kipaketi cha sumu kali na kunywa. Dawa inafanya apoteze fahamu na kipovu kuanza kumtoka. Daudi anapofika nyumbani anampata katika hali hii na ulevi unamtoka. Juu ya meza pana barua hii:

Mpenzi mume wangu Daudi,

Mzigo uliokuwa ukisema umekulemea nimeshakutulia. Nenda na unaowapenda. Walee vyema watoto wangu. Unyonge una mwisho. Wako maiti, Mtima.

(uk.26)

Barua hii ilitekeleza jukumu iliyokusudiwa kwani Daudi analia na kulia, kwa majuto. Anagundua kuwa bado anampenda mkewe sana na anitamani fursa ya ‘maiti’ afufuke amwombe msamaha na amwoneshe mapenzi aliyokuwa amemnyima wakati wote huu wa miaka saba.

Barua hii inatumiwa kumshutumu Daudi kwa madhila anayomfanyia mkewe na kama kigezo cha kushtusha mapenzi aliyokuwa nayo mbeleni.

Daudi alipokuwa analia kwa kekefu na uchungu mwingi, anahisi mkono umewekwa begani pake.

Anapogeuka anamkuta binti yake mkubwa Zamda kamsimamia na kibarua kingine mkononi. Anamfahamisha kuwa mamake alikuwa amemwagiza ampe yeye babake kibarua akimuona akilia. Daudi akakifungua na kusoma:

*Mpenzi mume wangu Daudi,
Pigo ni kupokezana. Waonaje maumivu yake? Mimi
nilikuwa nikiatilika kwa miaka kwa pigo la
mapenzi na mateso yako. Nimestahamili si haba.
Kwa kibarua hiki napenda kukuarifu kuwa mimi sijafa.
Nimekula dawa za kuzirai tu. Baada ya muda
fulani, nitafufuka. Waonaje tukafungua ukurasa mpya
wa mapenzi?
Wako wa daima,
Mtama.
(uk.27)*

Barua hii inampa Daudi nafasi nyingine katika maisha ya kuishi kama mtu na wala si mnyama. Barua hii inamrejeshia tumaini jipya katika maisha na baada ya barua hii, watu hawa wawili wanafungua ukurasa mpya wa maisha yao.

Katika hadithi ya ‘Nyuma ya Pazia’, Sheikh Majid anapokea barua fulani kutoka kwa Kassim anayejifanya yeye ni Maryam. Sheikh Majid alikuwa amemfuata Maryam kwa siku nyingi akitaka awe mpenzi wake. Kassim anataka kuthibitisha maneno haya ya unafiki wa Sheikh wake na kwa hivyo anamwandikia hii barua:

*Mpenzi Bwana Majid,
Watu wameshatamka, “Mstahamilivu hula mbivu”.
Lo, umestahamili si haba. Nakuonea huruma.
Nikikunyari kweli unanipenda, au unataka
kunionyesha ushehe wako tu? Lakini juhudi
zako zimenitambulisha dhati ya pendo lako.
Nikupe nini? Naacha uje unambie
mwenyewe kesho ufukweni Forodha ya Mchanga:*

saa tatu za usiku juu ya alama.

Anayekuthamini,

Maryam Abdulla

(uk.59)

Tamaa ya Sheikh Majid inamwongoza hadi ufukweni siku hii. Kassim anavaa buibui kama mwanamke asijulikane. Sheikh anapomwita ‘mpenzi’ na kumwambia atoe kizoro, anaaibika kwelikweli anapobaini kuwa ‘mpenzi’ ni Kassim, kijana aliyemshtumu kwa kupenda maji ya kitamali na kufanya mambo ya siri. Barua hii inatumika kama silaha ya kufichua unafiki wa Sheikh Majid wa kuwalaumu wengine ilhali yeye afanya maovu yale yale.

4.2.8 Nyimbo

Nyimbo ni maneno na sauti zilizopangwa na kupigwa kama ngoma ambazo huwa ni muziki. Nyimbo husaidia kujenga taswira fulani na kuibua maudhui mbalimbali. Mwandishi anatumia mbinu ya wimbo katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’. Katika kisiwa cha Pemba, machumi ya karafuu yanaleta furaha na misiba yake. Wapemba wanashuhudia mchezo wa ng’ombe wakati huu. Wakaazi wanajitayarisha siku hii kwa mavazi mapya na kufika uwanjani mapema kushuhudia mchezo baina ya ng’ombe na wanaume. Siku inapofika watu wanaelekea uwanjani kushuhudia Kipelele akichezewa na wanaume wanaoshika matambara au mibacha. Kipelele anatolewa uwanjani baada ya kutiwa hamaki. Hoihoi za wanawake zinasikika, kila mmoja anapaza sauti asikike na mpenzi wake akiwa uwanjani. Nyimbo za wanawake zinamiminika, ya Mwanamaua ikipanda juu kuliko za wote.

Wanawake wanaimba:

Na ugweo;

Na ugweo;

Simba mla nyama;

Akikosa mla nyama,

Akalili tunda ua.

Mwaka jana hajatoa pembe,

Mwaka huu kaja kashaota pembe

Salale kingwele!

Tachezwa n'nani?
Alo mbuyu wangu
Kacheze nimwone!
(uk.84)

Wimbo huu unampenya Dadi moyoni na kumtia wazimu na hamu ya kupigana na Kipelele. Wimbo huu unatumiwa kumpa ujasiri Dadi kumchezea Kipelele. Dadi anashindwa kujikinga na pembe za Kipelele anayemrusha juu na anapaonguka chini anamlalia, damu inamtoka Dadi puani na kinywani. Mwandishi anatumia wimbo huu kufanikisha anwani ya hadithi yake, 'Mhanga wa Mwanamaua' kwani Mwanamaua anamtoa kama kafara akitaka ujasiri wake utambuliwe na wanakijiji, hatima yake ni kumpoteza mchumba wake.

4.3. Hitimisho

Katika sura hii, tumechunguza matumizi ya lugha katika kiwango cha kisemantiki. Tumeangalia namna tamathali za semi zimetumiwa na Said A.Mohamed kwa ustadi mkubwa ili kuweza kufafanua maudhui kwa njia inayokuza uelewaji zaidi. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo tumechunguza ni pamoja na tashbihi, sitiari, kinaya, tashhisi, tanakuzi, majazi, tasifida, maswali ya balagha na chuku.

Pia tumechunguza mbinu za lugha kama vile takriri, usambamba wa visawe, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi, jazanda, methali, barua na nyimbo.

Mbinu hizi zimetumiwa kwa majukumu kadhaa. Zimetumiwa kufafanua maana, kuibua hisia mbalimbali, kuchekesha na kupamba lugha ya msanii na kuondoa ukinaifu wa lugha chapwa. Muhimu zaidi ni kuwa zimetumiwa kukuza na kutilia msisitizo maudhui ya Said A. Mohamed . Katika sura ya tano inayofuata, tumetoa hitimisho ya kazi hii.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumehitimisha utafiti wetu wa mtindo katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumetaja matokeo ya utafiti huu, umuhimu wa utafiti wetu na mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu diwani hii.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti wetu wa mtindo katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* umejikita katika viwango vitatu vya lugha. Viwango hivi ni msamiati, sintaksia na semantiki. Utafiti wetu umebaini kuwa Mohamed ni mkwasi wa lugha ya Kiswahili na ameitumia kwa ufundi mkubwa. Amemulika masuala tata yanayomkumba mja katika maisha. Masuala haya ni pamoja na majuto, misukosuko katika ndoa, kufanya kazi bila maoni, mkengeuko, unafiki katika jamii na dini, ukosefu wa haki, upweke, mapenzi, ukahaba na ulevi, miongoni mwa mengine.

Uchunguzi huu umebaini ukiushi wa aina mbalimbali alioutumia mwandishi katika kupitisha ujumbe kwa hadhira yake. Katika kiwango cha msamiati, tumetambua kuwa Mohamed ametumia uhuru wake wa kuunda msamiati mpya. Amechagua kutumia maneno ya lugha nyingine katika maandishi yake ya Kiswahili, matumizi ya msamiati wa Kipemba, uteuzi wa anwani za hadithi zinazolingiliana na maudhui, ukiushi wa maumbo na sajili mwafaka. Pia, kuna uteuzi wa msamiati mpya anaoutumia. Tumegundua kuwa msamiati anaoutumia mwandishi umefungamana na matukio na muktadha wa hadithi fupi zinazozungumziwa.

Katika kiwango cha sintaksia, kuna ukiushi wa kategoria za maneno yaani, nomino, vielezi, viunganishi, vihusishi na vivumishi. Tumegundua kuwa sababu kuu ya ukiushi huu ni kutilia mkazo hali au wazo fulani katika hadithi ili aafiki maudhui yake.

Utafiti wetu umewezesha kubainisha matumizi ya sentensi ndefu na fupi katika diwani hii. Sababu kuu ya sentensi hizi ni kuongeza au kupunguza mtitimo wa wazo au hali anayoshughulikia ili ioane na maudhui yake. Mbali na haya, utafiti wetu umeona kuwa, kuna ukiushi wa uakifishaji. Tumegundua kuwa msanii ametumia alama za dukuduku (...) kwa kiwango kikubwa katika hadithi zote kwa madhumuni tofauti na yale ya kawaida. Ukiushi huu unachimuza pakubwa na kuchangia kuathiri hisi za wasomaji mbali na kuongeza ujumi katika hadithi husika.

Mbali na haya pia tumechunguza sentensi zilizokiuka muundo wa kiima kiarifu. Mwandishi ametumia ukiushi huu kwa ustadi ili kubanisha upekee wake.

Katika kiwango cha semantiki tumeona kwamba, kuna ukiushi wa kimaana katika matumizi ya tamathali za usemi kama tashbihi, sitiari, kinaya, tashhisi, tanakuzi, majazi, tasifida, maswali ya balagha na chuku. Pia tumechunguza mbinu nyinginezo za lugha ambazo ni takriri, usambamba wa visawe, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi, jazanda, methali, barua na nyimbo. Tumethibitisha kuwa mbinu hizi zimetumiwa ili kuchochea hisia na kumpa msomaji taswira ya hali halisi ya mazingira ya hadithi hizi.

Katika kutambua ukiushi katika viwango vyote vitatu, nadharia tete yetu ya kwanza ya kuhakiki vipengele muhimu vya kimtindo ni ya kweli.

Utafiti wetu pia umebainisha jinsi mwandishi alivyotumia ukiushi huu kukuza maudhui yake. Kwa hivyo nadharia tete yetu ya pili iliyotaka tubainishe jinsi ukiushi wa vipengele vya kimtindo umeendeleza maudhui katika diwani hii ni ya kweli.

Katika kuonyesha uhusiano kati ya ukiushi wa mwandishi katika viwango vyote vitatu, tumefaulu kuonyesha uhusiano uliopo kati ya dhana hizi mbili na hivyo kuchangia katika uelewekaji wa hadithi katika diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tumebainisha muumano huu na hivyo kuthibitisha nadharia tete yetu ya tatu.

Nadharia yetu ya Elimumitindo imetufaa pakubwa katika kuhakiki mtindo katika diwani hii. Hii ni kwa sababu nadharia hii inahusu kubainisha sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi ya kifasihi na ambazo humtambulisha mwandishi wa kazi fulani.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tumethibitisha kuwa mtindo katika utanzu wa hadithi fupi haujashughulikiwa kama ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi kama riwaya na tamthilia. Hivyo basi, utafiti huu umetoa mwanga wa kuhakiki mtindo katika utanzu huu. Hii ni kwa sababu watafiti wa baadaye watakuwa wanarejelea mchango wa kazi hii kimtindo.

5.2 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti huu umejikita katika kipengele kimoja cha fani ambacho ni mtindo. Kuna vipengele vingine vya fani kama vile muundo, mandhari na wahusika. Vipengele hivivinaweza kufanyiwa utafiti hapo baadaye. Pia, utafiti huu umejikita katika ukiushi wa kimsamiati, kisintaksia na kisemantiki. Kuna viwango vingine vinavyoweza kutafitiwa kama vya kifonolojia, kimofolojia na hata kiwango cha kiusemi au kidiskosi. Kuna haja ya kutafitia vipengele hivi na kuonyesha mchango na athari zake katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*.

MAREJELEO

- Arege, T. M. (2007). *Kielezi cha Tungo*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Burhani, Z. (1989) *Mwisho wa Kosa*: Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- English-Swahili Dictionary, 3rd Edition* (2006). Dar es Salaam: Tuki.
- Habwe, J. na Matei A. (2006). *Darubini ya Kiswahili Marudio: Kamili ya KCSE*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Habwe, J. na Nyonje J. (2007). *Darubini ya Utunzi. Insha na Tungo Amilifu*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Kamusi ya Karne ya 21 (2011). Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Kihore, Y. na Wenzake (2000). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo Vikuu*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (TUKI) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kitali, H. N. (2011). “Fani na Usawiri wa wahusika wa kike katika Tamthilia ya *Pango na Mama ee*”. “Tasnifu ya M. A.” (Haijchapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kitsao, J. (1975). “A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts.”Tasnifu ya M. A. (Haijchapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi, Mtaala wa Kiswahili*. Nairobi: Kampala: Dar es Salaam: East African Literature Bureau.
- Leech, G.(1969). *A linguistic Guide to English Poetry*. New York: Longman Group Ltd
- Leech, G. na Short, M.(1981). *Style in Fiction: A linguistic Introduction of English Fictional Prose*. New York: Longman Group Ltd.
- Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mbatiah, M. (mh) (2000). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- _____ M.(2001). *Kamusi ya Fasihi*, Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*: Nairobi: East African Educational Publishers.
- _____ (2005). *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Nairobi. Longman Publishers Ltd.

- _____ (2005). *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Msokile, M. (1993). *Misingi Ya Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi: East African Educational Publishers.
- Ndung'u, N. (1996). "Uhakiki wa fani katika riwaya za Katama Mkangi: *Ukiwa, Mafuta na Walenisi*. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Obuchi, S. M. na Mukhwana A. (2010). *Muundo wa Kiswahili, Ngazi na Vipengele*. Nairobi: A~Frame Publishers.
- Ongarora, S. O. (2007). "Mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*". Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Otieno, N. O. (2005). "Muumano wa Leksika Katika Matini: *Babu Alipofufuka*" Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- _____ (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.